ZAWADI YA MUNGU ILIYOFUNGWA

Mbarikiwe . . .

Siku zote ni vema kuja katika Nyumba ya Bwana, lakini vema zaidi, inaonekana, katika hizi, ni Krismasi na Mwaka Mpya na sikukuu. Inaonekana kana kwamba ina baraka ndogo maalumu iliyosalia kwa ajili yetu. Ndipo wakati sisi . . . Ni vibaya sana tu kwamba hatuwezi kuwa na hisia hii ya Krismasi wakati wote. Watu wakikupungia mikono, na kusema, "Bwana akubariki." Hilo ni zuri. Napenda jambo hilo moja kuhusu Krismasi.

Sasa, nilikuwa nikisikiliza kusanyiko la Kesha likitangazwa, ninaamini, kwamba ni Jumamosi ijayo usiku. Bwana akipenda, nitajaribu kuwa hapa wakati huo, kwenye kusanyiko la Kesha, na kuchangia wakati wangu, Bwana akipenda, kuwasaidia kuzungumzia kidogo juu ya somo fulani Jumapili ijayo usiku. Halafu Jumapili asubuhi, hakika, ni shule yetu ya kawaida ya Jumapili. Nao usiku wa Jumapili ni ibada ya kiinjilisti. Sasa . . . [Ndugu Neville anasema, "Kutawadhana miguu, Jumapili ijayo usiku, pia."—Mh.] Naam. Ushirika, kutawadhana miguu, Jumapili ijayo usiku. Hiyo ni kweli. Njia nzuri ya kuanza Mwaka Mpya, kweli, kufanya ushirika, kutawadhana miguu.

Sasa, ninataka kufanya tangazo hili, ya kwamba ninauliza ya kwamba huu ni mkutano mdogo, maalum, tuseme, wa wachungaji tu na wachungaji washiriki wa maskani, wadhamini na mashemasi wa maskani hii. Nafikiri ni vema kwetu kukusanyika pamoja, mara moja moja, na kwa namna fulani kutafuta kujua jinsi Bwana anavyotuongoza. Na mara nyingi yapo mambo madogo yanayoibuka, kama vile Maandiko ambayo ungeweza kupata, ambayo yangekuwa ni magumu. Na endapo hatuninii . . . Tunataka vile vile, kuzungumza jambo lile lile, kila mahali. Pia tunataka kuja pamoja.

Nami ninawataka ninyi wachungaji na washiriki: Hakika, Ndugu Neville, hilo lingekuwa; na Ndugu Don Ruddell huku juu, mmoja wa washiriki wetu; na Ndugu Graham Snelling huko Utica; Ndugu Stricker hapa, mmishenari wetu; na to- . . . ndugu ambao ni wachungaji, Ndugu . . . hao mbalimbali hapa; Ndugu Parnell; nanyi mnajua washiriki ni akina nani hapa; Ndugu Junior Jackson, kutoka huko chini New Albany; halafu ma—mashemasi na wadhamini.

Nawaambia kile ningetaka mfanye. Juma hili lijalo, jichukulieni kipande kidogo cha karatasi, na mwandike mle ndani ma—mawazo ama ninii . . . ningesema, kwa Maandiko, ama wajibu fulani ambao inakubidi kushughulikia, ambao huenda ikawa hujui.

2 Kama vile mdhamini angesema, "Wajibu wangu ni upi kama kisa *hiki* kikiibuka?" "Kazi yangu ni ipi, kama shemasi, kama kisa *hiki* kikiibuka?" Naye mchungaji huenda akasema, "Katika Neno hili, *hapa*, ninaona ambapo lilipaswa kuwa *hivi na hivi*, na mimi—mimi sielewi jinsi tu tunavyolifundisha. Na kuliweka hilo chini katika Maandiko, na kadhalika." Kisha myalete yote, kwa Ndugu Wood, mkiweza, maana yeye anaishi mlango wa pili kutoka kwangu. Basi mara ukiliandika lako, na upesi uwezavyo, nitalithamini, kusudi niwe nikiliangalia katika Maandiko.

Nasi tutakuwa na huu. Sio. . .Haukuwa ni mkutano wa umma sasa. Ni wa wachungaji tu, na wa maskani hii, na mashemasi na wadhamini wa maskani. Na huo utafanyika mara moja, mara tu tunapoweza kuyaleta. Ndipo tutatangaza usiku mmoja ambapo ha—hakuna mikutano inyoendelea hapa, ndipo tu—tutaushughulikia huo basi.

3 Nafikiri lingekuwa ni jambo zuri, Ndugu Neville, ikiwa hao ndugu, ninyi nyote wachungaji, na kadhalika, kwamba tukusanyike pamoja. Hivyo tunaweza kuzungumza jambo lile lile, kila mahali, mnaona, tunajua. Halafu huo utarekodiwa, pia, maswali yetu na majibu yetu yatarekodiwa, na kila mmoja anaweza kupata kanda, kusudi mpate kujua, kuicheza tena, kukiwa na jambo lolote, swali lolote linaloibuka, lipate kuwa ni kwa manufaa ya kanisa. Ama mtu fulani angesema, "Vema, *hili*." Tutarudi nyuma tuone yaliyo kwenye kanda, vile ilivyosema. Tunazo kanda za namna hiyo, tayari. Na sasa tuna wadhamini wapya, nafikiri, mwaka huu, na—na mashemasi wapya, na kadhalika, nasi tunapenda wafunzwe juu ya hayo.

4 Naye maskini ndugu huyu, huyo ni mmoja wa ndugu zetu kutoka hapa juu Sellersburg, Ndugu Willard Crase, hakika mpasheni habari, mkiweza, kwa kuwa yeye ni mchanga tu katika Bwana. Pia—pia kama jamaa hawa wadogo, nafikiri, wanaweza kuimarishwa, mnaona ninalomaanisha, wajue tu jinsi ya kushikilia. Basi maswali madogo huibuka niani mwao. Badala ya kuchukua msimamo unaotofautiana na wengine, hebu tuje pamoja tu—tuone yote yanahusu nini. Ndipo wakati sisi. . .mikutano yetu, mikutano yetu mikuu, ya pamoja, wakati makanisa yanapoungana, kama vile tumekuwa katika kipindi hiki cha mwisho, ndipo tu—tungejua tu tuchukue nini, na la kusema, kile tu cha kufanya. Sote tunataka kuzungumza lugha ile ile, tupate kufahamu.

5 Sasa, jambo lingine ningependa kusema. Kama vile Ndugu Neville amesema vizuri kwamba, tunawatakia heri kwenye habari hizi njema za Krismasi katika wakati huu wa—wa ushirika kwenye sikukuu hizi, na kadhalika.

6 Kisha ninataka kuchukua wakati huu kuelezea, kwa kila mmoja wenu, jinsi ninavyowashukuru, kwa ajili ya kadi zenu za Krismasi na zawadi, na vitu vilivyopokelewa nyumbani mwetu.

Bila shaka ninawashukuru, kwa moyo wangu wote. Hakika lilitufaidi, asubuhi ya leo. Wakati . . . Ninaye mvulana mdogo, mdogo vya kutosha kwa namna fulani kutaka mti wa Krismasi, nasi tulikuwa nao chumbani. Basi asubuhi ya leo, nilienda kule chini, nikakuta zawadi kadhaa kutoka kanisani mwangu hapa, na marafiki zangu kutoka sehemu mbalimbali, zilizokuwa zimeingia, zimewekwa chini ya huo mti. Nami sina maneno ya kuwaelezea kile mimi . . . jinsi ninavyothamini kila moja ya hizo. Basi Mungu wa Mbinguni na awabariki sana, ndilo ombi langu. Na sasa . . .

7 Nasi, mnajua jinsi ingekuwa, hatuwezi kutuma zawadi pia, kwa sababu kamwe nisingeweza kupata kiasi hicho cha fedha, mwajua. Ni—ninapata dola mia moja kwa juma, nami ninayo familia kubwa, na yapata marafiki milioni kumi, na hakika kidogo ingekuwa ni vigumu kuwazawadia wote. Lakini tu—tunawashukuru pamoja na mawazo yenu. Nami nina hakika mnaelewa.

8 Sasa msisahau huu—usiku huu ujao wa Mwaka Mpya. Loo, nakumbuka mkutano wa Kesha ya kwanza niliyopata kuwa nayo hapa kwenye maskani hii. Sidhani kuna mtu yeyote hapa anayeikumbuka. Lakini huo ulikuwa ni usiku mmoja Bwana aliondoa ugumu mwingi sana kutoka kwa mchungaji wenu. Kwa hiyo, tunatarajia wakati mkuu basi.

9 Na sasa, kabla tu hatujaomba, ningetaka kusoma somo la Maandiko usiku wa leo.

10 Na kidogo nimekuwa nikijadiliana na nafsi yangu leo hii. Ni—nilitangaza ya kwamba nilikuwa ninaenda kuzungumzia, usiku wa leo, kama nikifika hapa, *Tumeiona Nyota Yake Mashariki*, *Nasi Tumekuja Kumsujudia*. Huo kidogo unasikika unajulikana kwangu. Ndipo rafiki yetu mwema, Ndugu Sothmann hapa, nanii . . . mmoja wa wadhamini wa kanisa, nilimwuliza. Naye akasema, "Ninayo kanda yake, Ndugu Branham. Uliuhubiri, mahali fulani." Naye rafiki yetu wa thamani, Ndugu Leo Mercier hapa, mvulana wa kanda, akasema, "Naam, yapata mara tano." Kwa hiyo, ni—nikaubadilisha kidogo tu. Basi badala ya kuhubiri juu ya *Tumeiona Nyota Yake Mashariki,* ninataka kuzungumzia somo, usiku wa leo, la: *Zawadi Ya Mungu Iliyofungwa*.

11 Na sasa nitasoma kutoka kwenye Injili ya Mathayo Mtakatifu, m—mlango wa pili, kwa ajili ya somo la Maandiko, mlango wa pili wa Mathayo Mtakatifu.

> *Yesu alipozaliwa katika Bethlehemu ya Uyahudi zamani za mfalme Herode, tazama, mamajusi wa mashariki walifika Yerusalemu,*
>
> *Wakisema, Yuko wapi yeye aliyezaliwa Mfalme wa Wayahudi? Kwa maana tumeiona nyota yake mashariki, nasi tumekuja kumsujudia.*

Basi mfalme Herode. . .aliposikia hayo, alifadhaika, na Yerusalemu pia pamoja naye.

Akakusanya wakuu wa makuhani wote na waandishi wa watu, akatafuta. . .kwao, Kristo azaliwa wapi.

Nao wakamwambia, Katika Bethlehemu ya Uyahudi: kwa maana ndivyo ilivyoandikwa na nabii,

Nawe Bethlehemu, katika nchi ya Uyahudi, *hu mdogo kamwe katika majumbe wa Yuda: kwa kuwa kwako atatoka Mtawala, atakayewachunga watu wangu Israeli.*

Kisha Herode akawaita wale mamajusi faraghani, *akapata kwao hakika ya muda tangu ilipoonekana ile nyota.*

Akawapeleka Bethlehemu, akasema, Shikeni njia, mkaulize sana mambo ya mtoto; na mkiisha kumwona, nileteeni. . .habari tena, *nileteeni habari tena, ili mimi nami niende nimsujudie.*

Nao waliposikia maneno ya mfalme, walishika njia; na, tazama, ile nyota waliyoiona mashariki, ikawatangulia, hata ikaenda ikasimama juu ya mahali alipokuwapo mtoto.

Nao walipoiona ile nyota, walifurahi furaha kubwa mno.

Wakaingia nyumbani wakamwona mtoto pamoja na Mariamu mamaye, wakaanguka wakamsujudia;. . . walipokwisha kufungua hazina zao, nao *wakamtolea tunu;* za *dhahabu. . .uvumba, na manemane.*

Nao wakiisha kuonywa na Mungu katika ndoto wasimrudie Herode, wakaenda zao kwa njia nyingine.

12 Sasa nataka kuchukua somo kutoka hapo, usiku wa leo. Ama, sio kutoka hapo, bali kutoka kwenye hadithi hiyo hiyo, katika Luka Mtakatifu 2:7.

Akamzaa—akamzaa mwana, kifungua mimba, akamvika nguo *za kitoto, akamlaza katika hori ya kulia ng'ombe; kwa sababu hawakupata nafasi katika nyumba ya wageni.*

13 Hebu na tuinamishe vichwa vyetu sasa kwa maombi.

14 Mungu mtakatifu na mwenye neema, Yule aliyetupatia Zawadi iliyo kubwa kuliko zote ambayo ulimwengu huu umewahi kujua, Bwana Yesu Kristo, kwa unyenyekevu tunakuja Kwako, usiku wa leo, katika shukrani, na kuonyesha kutoka kwa utu wetu wa ndani kabisa, ibada ya kilindi cha moyo wetu, Kwako, kwa ajili ya Zawadi hii ya ajabu sana. Hatuna kitu cha kutoa kama malipo. Nawe ulichoomba ni kidogo sana; hasa, "Njoni Kwangu, ninyi nyote msumbukao na mliolemewa

na mizigo mizito, nami nitaichukua mizigo yenu na dhambi zenu, na kuwaweka huru." Loo, ni badilisho la jinsi gani! Hakuna mtu angaliweza kufanya hivyo ila Wewe, Baba yetu. Nasi tunakushukuru ya kwamba Wewe umetufanyia jambo hilo. Nasi ni mashahidi Wako katika saa hii, ya kwamba Wewe unachukua mizigo yetu na dhambi zetu, na kutupa furaha na amani, badala yake. Jinsi tulivyo na shukrani, Bwana, kwa ajili ya ujuzi huu wa kindani wa Kikristo, Krismasi mioyoni mwetu. Tunashukuru sana kwa ajili ya jambo hili. Tuna furaha sana kujua ya kwamba tunaishi katika siku ya mwisho, wakati tunapoona ishara zikija tena kama ilivyokuwa katika siku hiyo, ya kakaribia Kwake. Tunainyenyekeza mioyo yetu katika Uwepo Wako, Ewe Uliye Mtukufu. Jalia Roho Wako atawale kabisa moyoni mwetu, maishani mwetu. Na ututie nguvu, kutoka ndani kwenda nje, tupate kuwa watumishi Wako, katika saa hii iliyo kuu na yenye giza ambayo ulimwengu sasa unaikabili.

15 Tunawasilisha kusomwa huku kwa Neno Lako, Bwana, Kwako, kwa kusudi hili moja, kwamba, kutoka kwenye Hili, Roho Mtakatifu aweze kuleta pamoja muktadha ambao ungekuwa ni wa kutosha, usiku wa leo, kama Ujumbe wa Krismasi kwa watu Wako wanaongojea. Nasi tunakungojea Wewe. Bwana, itahiri midomo itakayonena, na masikio yatakayosikia. Na utupe nguvu, na kutia Uhai katika Maneno yanayotolewa, yapate kutufikisha kwenye ufahamu bora wa Bwana Yesu. Kwa kuwa tunaomba katika Jina Lake. Amina.

16 Nimeandika Maandiko mengi hapa ya kurejea, na kadhalika. Nilishangazwa, jana, niliposikia hilo. Nilichukua gazeti, na kwamba kuna, kile ulimwengu wa biashara unachoita, "Krismasi kubwa mno," ambapo palikuwa na pesa nyingi zaidi zilizotumiwa wakati huu kuliko zilizowahi kutumiwa katika miaka mingi, mingi sana, tangu huko nyuma kabisa miaka mingi iliyopita. Na kwamba halaiki ya watu ilikuwa imekusanyika Yerusalemu, na jinsi ambavyo kulikuwako na kipindi kidogo cha amani kati ya Waarabu na Wayahudi, hata kidogo waliachilia hisia zao, wapate kuwaruhusu wa—wasafiri waingie mjini tena, kwenye msimu huu wa—wa Krismasi.

17 Mara nyingi nimeshangaa ni kwa nini mji huu ulipata kuchaguliwa, Bethlehemu.

18 Kama vile jamaa hao walivyoimba dakika chache zilizopita, hu—huyo jamaa mdogo na mkewe, na watoto. Na hapo nilishangaa, nikimtazama huyo msichana mdogo, jinsi alivyokuwa akidumisha wakati pamoja na hiki, namna fulani ya kinubi cha nyuzi ambacho alikuwa akikicheza. Na jinsi maskini jamaa huyo alivyokuwa angali tu ni mtoto mchanga, kabisa, lakini hata hivyo alikuwa akidumisha wakati tu pamoja na . . . ama kukichukua kinubi hiki. Nadhani kiliitwa kinubi. Sasa, ndipo mimi . . .

19 Tukiwaza juu ya Bethlehemu, na ni kwa nini ikawa kwamba ulichaguliwa kuwa mahali pa kuzaliwa Mfalme wa wafalme? Pia, mwajua, Bethlehemu ni mahali padogo, mji mdogo sana. Mara nyingi nimeshangaa ni kwa nini Mungu hakuchagua mahali pa kidini zaidi kwa ajili yake, kwa ajili ya tukio hili kuu, kama vile Shilo. Shilo ulikuwa ndio mahali pa kwanza ile hema, lile sanduku lilipowekwa, baada ya kuvuka Yordani. Ama Gilgali, mji mwingine mkuu wa kidini; ama Sayuni, mlimani, mji mwingine mkuu wa kidini; ama hata mji ule mkuu unaojigamba, Yerusalemu, pamoja na wenye hekima wake wote na watakatifu kote katika wakati. Ni kwa nini Mungu hakuuchagua Yerusalemu?

20 Ni kwa nini auchague Bethlehemu? Labda ilionekana kana kwamba huenda akapachagua mahali, moja ya ile miji mikuu ya kimbilio, ambayo ingemlinda Mwanawe ikiwa kwamba tatizo fulani lilitokea. Mahali pa kimbilio kama vile Ramothi-giliadi. Huo ulikuwa ni kimbilio kuu lililojengwa, kwa kuwa watu wangeweza kuikimbilia minara hii. Kadeshi ulikuwa ni mji mwingine mkuu wa kimbilio. Hebroni, mji mwingine mkuu wa kimbilio.

21 Kwa nini Mungu akauchagua Bethlehemu mdogo, halafu hakuichagua miji hii mikubwa zaidi? Nayo ilikuwa na majina makuu zaidi, na msingi mkubwa zaidi wa kiroho.

22 Lakini, mwajua, Mungu anayo njia ya kufanya mambo, njia Yake Mwenyewe tu kuhusu mambo. Nina furaha sana anayo. Mnaona? Wakati mwingine Yeye huchagua vitu ambavyo havina msingi wa kiroho, ama visivyo na msingi wowote hata kidogo. Basi hiyo ndiyo sababu Yeye ni Mungu; Anaweza kuchukua kitu ambacho si kitu, na kufanya kitu fulani kutoka kwake. Na, hilo, hilo ndilo linalomfanya Mungu. Hilo ndilo linalotufanya tumpende. Hilo ndilo linalotufanya sisi maskini kumfurahia, kwa sababu kwamba hata ingawa sisi, maskini, wasio na msingi, hata hivyo Mungu anaweza kufanya mambo pamoja nasi kama akiwahi kutuweka chini ya mamlaka Yake.

23 Yoshua, hakika, alikuwa ndiye aliyewavusha wana wa Israeli, na kuigawa nchi. Nalo kabila hili la Yuda lilipewa sehemu hii ilipo Bethlehemu, iliyo katika kona ya juu ya kaskazini mwa Yuda, kishoroba kidogo ambacho kwa namna fulani kinatokeza kama mkono mdogo wa nchi. Na katika mahali hapa, jimbo hili, jimbo hili kuu, ni nchi ya kaskazini ya ngano, ulikokuwa ule ukanda wa ngano, ambako wanalima ngano nyingi na shayiri.

24 Na mmoja wa wana wa Kalebu aliimarisha na kuanzisha mji huu. Jina lake lilikuwa Salmoni, alikuwa ni mmoja wa wana wa Kalebu. Ukitaka kulichunguza hilo, ninaruka mengi ya Maandiko haya, bali ninaona baadhi ya ndugu wanayaandika. Katika Mambo ya Nyakati ya Kwanza 2:15- . . .Pia, ungelipata

katika Mathayo 1:5. Na ambapo wao, aliuimarisha na kuuanzisha mji huu mkuu, ambao ulikuwa ni mji mdogo, bali ni mkuu kwa sababu ya mambo makuu yaliyotukia kwenye mji huu.

25 Kama vile nimesema daima, sio kanisa kuu; ni Mungu mkuu katika kanisa. Sio mlima mkuu, mtakatifu; ni Roho Mtakatifu mkuu aliyekuwa juu ya huo mlima. Sio mtu mtakatifu; ni Roho Mtakatifu ndani ya mtu huyo. Mnaona?

26 Hivyo ndivyo mji huu ulivyokuwa. Ulikuwa ni mdogo wa kimo, na zaidi sana katika bonde, wala haukuwa mzuri sana wa kutazama. Idadi yake ya watu ilikuwa ni ndogo, na ingali ni ndogo leo hii. Lakini ni kwa sababu Mungu aliuchagua kufanya jambo fulani. Hicho ndicho ninachokipenda, kitu ambacho Mungu huchagua. Haijalishi kinaonekana vipi, kwa watu, maadamu tu Mungu amekichagua.

27 Rahabu kahaba, ambaye sote tunamfahamu, yeye akiwa m—msichana mdogo aliyeachiliwa mtaani na baba na mama yake makafiri, waliomweka mtaani kwa kuwa alikuwa ni mrembo, na alikuwa alete mapato kwao, kwa ukahaba. Na hata hivyo, ndani ya msichana huyu mtovu wa uadilifu aliyeachiliwa mtaani, yeye alikuwa amesikia ya kwamba kulikuwako na Mungu Ambaye alijibu maombi. Basi nafasi ya kwanza aliyopata, kumkubali Mungu huyo ama kumfanyia jambo fulani, yeye alilifanya. Ndipo Mungu akayaokoa maisha yake, na kuwaokoa baba na mama yake, na familia yake. Alipendana na jemadari katika jeshi la Israeli, tunaona katika historia, naye akaolewa na jemadari huyu. Nao uchumba wao ulikuwa ni mzuri sana. Ndipo hatimaye wakatulia na kuishi katika Bethlehemu.

28 Basi kupitia kwa jemadari huyu yeye alimleta ulimwenguni mwa—mwana, mwana wa—wa—wa. . . siwezi kukumbuka jina la jemadari huyo sasa hivi, nilikuwa nikijaribu kulikumbuka. Nilifikiri nilikuwa na jina lake hapa chini, bali sina. Ninalo jina la mwanawe, bali ilikuwa ni mwana wa Rahabu kwa jemadari huyu. Jina lake lilikuwa ni Salmoni. Sio Sulemani aliyelijenga hekalu, mwana wa Daudi. Bali, mwingine, Salmoni, naye Salmoni huyu akamzaa mwana ambaye jina lake lilikuwa ni Boazi. Naye Boazi, loo, sote tunaifahamu hadithi hiyo ya ajabu ya Boazi na Ruthu.

29 Sasa, mnaona, kahaba huyu alikuwa ni Mmataifa, naye alikuwa ni nyanya wa kale wa Bwana wetu Yesu. Na pia wakati—wakati Boazi, mjukuu wake, alipojitokeza na kumwoa Ruthu Mmoabu, yeye pia alimwoa Mmataifa. Ambalo lilimfanya Yesu pia nusu Mmataifa, tukinena kidunia. Basi walipomzaa mtoto wao, jina lake lilikuwa ni Obedi. Naye Obedi alikuwa na mwana, nalo jina lake lilikuwa Yese. Naye Yese alikuwa na mwana jina lake Daudi. Yote haya yalitukia katika Bethlehemu mdogo. Ni kitu gani? Ukoo wa Bwana Yesu, msingi Wake ambao wale watu

mashuhuri wa kiroho walikuwa wakiupuuza, ama waliojiita watu wa kiroho.

30 Na ilikuwa ni kwenye ardhi ii hii ambapo nabii Samweli alimpaka Daudi mafuta kuwa mfalme juu ya Israeli, papa hapa Bethlehemu. Na kupitia Daudi akaja yule Mwana mashuhuri, "Ewe Mwana wa Daudi," Mwana aliyezaliwa katika hori dogo la zizi huko karibu na kilima, upande wa magharibi mwa huo mji. Ilikuwa ni kule juu ya kilima hicho ambapo Malaika wa Bwana waliimba noeli yao ya kwanza.

31 Neno Bethlehemu, hebu tulichambue. B-e-t-h linamaanisha "nyumba." E-l linamaanisha "Mungu." E-l-h-a-m linamaanisha "Mkate." "Nyumba ya Mkate wa Mungu." Jinsi lilivyofaa basi kwa Mkate wa Uzima kutoka Bethlehemu, "Nyumba ya Mkate wa Mungu." Loo! Ni hadithi tamu.

32 Hapana shaka ilikuwa kidogo tu baada ya giza kuingia, nalo jua lilikuwa limetua. Nyota huenda ikawa zilikuwa zimetokeza, nayo nuru ilikuwa imeondoka yapata muda wa saa mbili. Wakati maskini yule punda alipokuwa akiweka miguu yake midogo, michovu juu kupitia upande wa nyuma wa kile kilima, magharibi mwa Bethlehemu, wakati akiangalia mahali alipoziweka maskini kwato zake, kwa sababu mzigo wake ulikuwa ni wa thamani. Naye Yusufu alikuwa akimwongoza kwa upole, huku maskini hao watatu walipoanza kupanda hicho kilima, ama walikuwa wakisafiri siku nzima, wakipanda kutoka huko chini kwenda Nazareti. Naye alikuwa akitarajia kujifungua wakati wowote, wakati umepita sana, labda.

33 Lakini mambo yote yamekusudiwa tangu zamani na Mungu, ambayo hufanya kazi kwa manufaa ya wale wampendao. Ilikusudiwa na Mungu ya kwamba kunapaswa kuwe na mfalme katili siku hizo, Herode mwuaji. Mungu alijua kuhusu hilo. Mungu alijua juu ya hizo kodi, na jinsi ambavyo serikali hii ya kinyama haikuwa na mawazo ya rehema juu ya maskini mama huyo ambaye alikuwa karibu tu kujifungua mwanawe kifungua mimba, katika siku chache tu. Bali aliagiza, ya kwamba, "Wote wanapaswa kuja mahali walipozaliwa, na kulipia kodi. Haidhuru yuko katika hali gani, hana budi kuja, kwa vyovyote vile." Mungu alijua yote kuhusu hayo. Alijua mambo yote tangu zamani. Na Yeye—Yeye anajua mambo yote, mnaona, Naye anafanya kila kitu kufanya kazi kwa manufaa.

34 Maskini hao watatu hawakuwa wakililalamikia, wakati wakipanda kile kilima. Hatimaye, baada ya kuugua kwingi, maskini yule punda, ninaweza kuwaona wakati wangesimama juu ya kile kilima; mahali ambapo . . . wakija kutoka upande wa magharibi, kutoka Nazareti, akipanda. Basi wakiisha kufika juu ya kile kilima, kuangalia chini bondeni palipokuwapo Bethlehemu mdogo. Mienge mingi ilikuwa ikiwaka. Watu wengi walikuwa wamekusanyika kutoka kote Galilaya, kuja kwenye

mahali pao pa kuzaliwa kule Bethlehemu, na kupitia kwenye huo mkoa, wapate kutozwa kodi na serikali ya Kirumi. Haijalishi hali zilivyo, waling'ang'ania barabarani, wagonjwa na wahitaji, na wagonjwa kitandani, wenye ukoma, wenye kansa, ma—ma—ma—maskini, walemavu, vilema, vipofu. Wote ilibidi waje, kwa sababu ilikuwa ni amri ya serikali. Naye Herode alikuwa nyuma yake, na halina budi kutekelezwa.

35 Basi wakati maskini kikosi chetu kinaposimama juu ya kile kilima, hapana shaka palikuwapo na jiwe kubwa limewekwa pale. Nami ninaweza kumwona Yusufu akimchukua, kwa upole, mikononi mwake, na kumsaidia kushuka kwenye maskini yule nyumbu, na—na kumweka kando ya hilo jiwe. Ndipo maskini yule nyumbu akavuta pumzi yake. Ndipo wakati Yusufu basi alipopiga hatua chache mbele, akauangalia Bethlehemu mdogo, aliona mitaa imejaa watu, na makelele, na mienge ikiwaka mitaani, na mayowe ya hao watu. Nao walikuwa wamelala viwanjani na nyuani, na wote nje ya malango ya huo mji. Hapana shaka ilikuwa ni tamasha kwelikweli!

36 Hapana shaka Yusufu alisema kitu kama hiki. "Mariamu, mpenzi, wazia tu. Ng'ambo tu ya mji huu, upande wa kaskazini, hapo ndipo Ruthu Mmoabu alipookota masazo kwenye mashamba ya Boazi. Huko, ng'ambo tu ya hapo, huko juu kwenye ule mlima, ndiko Daudi, pamoja na kombeo lake, alipombwaga simba chini, na kumnyakua kondoo kutoka kinywani mwake. Hapana shaka ilikuwa ni pale, ambapo Yoshua alisimama hapa na upanga wake uliometameta, yule shujaa shupavu wa watu wetu, akaigawanya nchi, na kulipa urithi huu kabila la Yuda, ambalo, kipenzi, sisi ni wa ukoo wake." Na kwenye mambo mbalimbali, ya vile hapana shaka alikuwa akimwelezea yale yaliyotukia.

37 Ndipo kwa kutosikia sauti yoyote nyuma yake, hapana shaka aligeuka kuangalia, aone iwapo angali alikuwa ameketi juu ya lile jiwe. Basi alipogeuka, na kuuona uso wake mrembo umegeuzwa kuelekea angani, haikumbidi kuuliza tena, kwa kuwa uakisi wa ile Nyota ulikuwa ukiangalia nyuma kupitia machoni mwake. Alijua alikuwa akiangalia kitu Fulani.

38 Ndipo akamwangalia, na kusema, "Yusufu, hivi umeiona ile Nyota inayoning'inia kule?"

39 Basi alipoangalia, na ule mshangao, kasema, "Sikuwa nimeiona hapo awali, mpenzi."

40 "Vema, imekuwa ikitufuata tangu jua lilipotua. Nimeiangalia. Hapana shaka inamaanisha jambo fulani, kwa sababu ninayo hisia ya ajabu sana."

41 Mwajua, Mungu hufanya mambo kama hayo, wakati mwingine, kwa ajili ya watu Wake, anatuonyesha Nuru, ama njia fulani ili tuweze kujua ya kwamba Yeye yuko karibu na yuko jukwaani. Haidhuru ulimwengu unasema nini au kufanya

nini, Yeye angali pale, na kila kitu kitakuwa shwari. Yeye analishuhudia tu tena, kwa Roho Mtakatifu, ili tuweze kumhisi.

42 Naye Yusufu hapana shaka alisema kitu kama hiki. "Mariamu, unajua nini? Sijawahi kuwa na furaha hivi maishani mwangu mwote. Wakati, nimesukumwa huku na huku na serikali ya Kirumi, lakini hata hivyo sijawahi kuwa na furaha kama niliyo nayo sasa hivi, wala sijui ni kwa nini. Inaonekana kana kwamba kuna utakatifu fulani juu ya maskini huu mji mdogo, usiku wa leo, ambako tulitangatanga tulipokuwa wavulana na wasichana, huko nyuma katika utineja wetu na umri wetu wa shule."

43 Huko mbali Mashariki, na mamia mengi ya maili kutoka hapo, Mamajusi tayari walikuwa njiani wakija. Walikuwa wameiona Nyota Yake, nao walikuwa wakija kukisujudu maskini Kifurushi cha Zawadi ya Mungu ambacho alikuwa akikituma ulimwenguni.

44 Kitambo kidogo tu kutoka hapo, nao ulimwengu ulikuwa unaenda kupokea Zawadi yake iliyo kuu kuliko yote uliyowahi kupokea, Kifurushi kidogo kilichofungwa. Kifurushi kidogo cha kwanza cha Krismasi, kilichowahi kufungwa, ulimwenguni kote, Mungu alikifunga. Ninataka kukatiza wazo langu, na kusema hivi. Kitu kikuu kuliko vyote kilichowahi kufungwa katika mwili wa mwanadamu kilikuwa kimefungwa ndani Yake. Mungu Mwenyewe alijifunga Yeye Mwenyewe katika kifurushi cha Krismasi na kukituma ulimwenguni.

45 Ni kwa nini wakakikataa Hicho? Kwa nini hawakukiona? Kwa nini wakakikataa Hicho? Ni kwa nini hawakukitaka? Sababu ile ile hawakitaki usiku wa leo. Hawakukabidhiwa katika desturi waliyozoea kupewa zawadi. Hiyo ndiyo sababu ingali imekataliwa, usiku wa leo, ni kwa sababu haijakabidhiwa watu katika desturi ambayo wamezoea kupokea zawadi.

46 Lakini Mungu hufunga Kifurushi Chake Mwenyewe. Yeye anayo haki ya kufanya hivyo, Yeye Ndiye anayeitoa. Anayo haki ya kukifunga kwa njia yoyote anayotaka kukifunga. Haileti tofauti yoyote jinsi ilivyo, Yeye anayo haki ya kulifanya kwa kuwa Ndiye anayetoa hiyo—hiyo Zawadi.

47 Jambo lingine, sababu yake ilikuwa, kama ilivyokuwa wakati huo, kwa vile haikuwa ni kawaida kwao kuipokea jinsi ilivyofungwa. Walikuwa wakitarajia kitu fulani, zawadi ije, ambayo ingeshuka kwa magari ya farasi, pamoja na ulinzi wa Malaika wakiendesha farasi wa moto. Lakini ilipokuja kama Mtoto mchanga akizaliwa katika hori, kamwe hawakujua Maandiko yalisema, "Nitaupa ulimwengu huu ishara kuu."

48 Waliomba wapewe ishara, siku moja. Yeye akasema, "Nitawapa. Itakuwa ni ishara kuu. Itakuwa ni ishara itakayodumu katika vizazi vyote. Bikira atachukua mimba na kumzaa Mtoto, Mwana, nao watamwita Jina Lake 'Imanueli.'

Hiyo ndiyo ishara kuu. Hiyo ndiyo Zawadi nitakayotoa." Bali haikuja kwa njia waliyokuwa wakiitarajia, nao wakaikataa.

49 Ndivyo ilivyo usiku wa leo, ndugu yangu. Karama ya Mungu haijaja jinsi watu wanavyoitaka ije, na kwa hiyo wameikataa. Hawaitaki. Wanataka ifungwe katika vitambaa wanavyotaka ifungiwe. Wanataka mapambo juu Yake. Wanataka kitu fulani kilichopambwa, kitu ambacho kimenakshiwa, kitu ambacho kinametameta, kitu ambacho ni maarufu. Lakini Mungu haitumi wakati wote jinsi hiyo. Yeye huituma katika nguvu, jinsi anavyotaka kuituma.

50 Jambo jingine, ililetwa na maskini. Mariamu, na Martha—Martha, hasa, ama . . . Mariamu na Yusufu walikuwa watu maskini sana. Walikuwa wakulima wadogo. Na kwa sababu ililetwa na maskini, hawakuitaka.

51 Ndivyo ilivyo leo hii. Wakati Zawadi hii kuu ya Kanisa, Roho Mtakatifu, anapowashukia maskini na wanyenyekevu, matajiri hawaitaki. Hawataki kujinyenyekeza. Wanaitaka pamoja na tabaka, bali hawaitaki jinsi Mungu anavyoituma. Watu wengi wanataka kumpokea Roho Mtakatifu, bali—bali wanataka kumpata jinsi watakavyo. Lakini, loo, ninashukuru sana kwamba huwezi kulifanya jinsi hiyo. Huna budi kulifanya jinsi Mungu anavyokutumia, na kujinyenyekeza ili tumpokee.

52 Hakuvikwa kwa kitani nzuri. Alivikwa nguo za kitoto. Ambazo, nimefundishwa kwamba kitu chenyewe ambacho Yesu alivikwa, yule Kristo, kilikuwa ni kitu kilichotolewa nyuma ya nira ya maksai, kilichoning'inia humo zizini. Yeye alivikwa nguo za kitoto, zilikuwa ninii—ninii . . . ambapo waliweka ninii . . . kitambaa shingoni mwa nira ya maksai, kuizuia isije ikasababisha lengelenge wakati akivuruta. Wao, wao hawakuwa na nguo kwa ajili Yake. Na wao . . . Loo, ninapowazia hilo, karibu linauvunja moyo wangu; hakuna nguo kwa ajili ya Imanueli, Muumba wa Mbingu na nchi. Wala hakuna nguo kwa ajili Yake kuvalia, ndipo ikambidi kuvikwa kitambaa ambacho maksai alikuwa amekitumia shingoni mwake. Loo, ni ishara kuu jinsi gani!

53 Inapaswa kuwa ya kuvutia sana kwa watu. Maskini Yehova, akilia kama mtoto mchanga. Mungu, aliyefanyika mwili, katika Kifurushi. Mungu, Ambaye hufunika anga lote na wakati, aliyekuwako kabla hapajakuwapo na ulimwengu, wala nyota, wala molekuli, amejifunga Mwenyewe katika Kifurushi kidogo na akalazwa horini; katika zizi, penye samadi ya ng'ombe na kondoo, na kadhalika; huko juu ya zizi, na katika zizi hili dogo, juu ya mabua ama majani makavu. Yehova alikuwa amelala pale, akilia kama mtoto mchanga. Mnaweza kuliwazia?

54 Mbona, matajiri hawakutaka kitu kama hicho. Hicho kingeyachafua mawazo yao wenyewe, kitu chochote kinyenyekevu jinsi hiyo. Naye angeletwa na msichana, mkulima

mdogo msichana aliyehesabiwa, katika ujirani wake, m—mlokole; na seremala ambaye labda alizijua ABC zake. Nao wangewezaje kamwe kuleta kitu ambacho kingeyavutia ama kuyaridhisha macho ya watu mashuhuri? Wangewezaje kamwe kutoa kitu ambacho kingewafurahisha ama kuwaridhisha matajiri, watu wenye kujivuna, ama madhehebu ya siku zao? Walikataliwa, kabisa.

55 Sio tu katika siku hizo, bali katika siku hizi, pia. Wanaikataa, kabisa. Haiji imefungwa jinsi wanavyoitaka. Wanataka ku—kuitupa, waseme, "Haina chochote." Kwa hiyo matajiri na madhehebu wanaikataa Zawadi hiyo. Hawakuwa na uhusiano wowote nayo. Kwa nini? Kwa nini wafanye jambo kama hilo? Haikuwa imefungwa katika desturi ya kanuni zao za imani. Hiyo ndiyo sababu kwamba, siku hizi, kwamba hawaitaki Zawadi ya Mungu. Marekani hii haimtaki Mungu. Makanisa haya hayamtaki Mungu. Wanamtaka Baba Krismasi. Wanataka kitu kilichopambwa na chenye rangi nyekundu, na—na—na—na kiangavu, kinachong'aa. Wanaikataa Kweli ya Injili, ya Nguvu na kufufuka kwake Kristo Yesu. Haitafungwa kwa kanuni zao za imani. Huwezi kumfunga Kristo katika kanuni ya imani.

56 Nilikuwa nikisikiliza, asubuhi ya leo, nilipokwa nikishuka kwa mama, mapema, nikaifungua redio. Na ka—kanisa fulani lilikuwa likinukuu ama kukariri ninii. . . kinachoitwa, Kanuni ya Imani ya Mitume. Hakuna kitu kama hicho.

57 Kanuni ya pekee mitume walijulikana kuwa nayo, inapatikana katika Matendo 2:38, "Tubuni, kila mmoja wenu, mkabatizwe katika Jina la Yesu Kristo, kwa ondoleo la dhambi zenu. Mtapokea kipawa cha Roho Mtakatifu." Hiyo ndiyo kanuni pekee ya imani niliyopata kuona, katika Biblia, waliyopata kutumia.

58 Hii nyingine ni kanuni ya kujibunia. Wala huwezi kumfunga Kristo katika kanuni ya imani ya Kipresbiteri, ama katika kanuni ya imani ya Kibaptisti, ama kanuni ya imani ya Kikatoliki, ama kanuni ya imani ya Kipentekoste. Kitu kimoja tu ambacho Kristo atafungwa kwacho, na hicho ni moyo wako, si kanuni yako ya imani. Yeye anautaka moyo wako. Yeye ana mnara wa kuongozea pale anaopenda kufanyia kazi pamoja nawe, kukuleta kwenye Uzima wa Milele. Yeye kamwe hatakubali; wala huwezi kumfunga katika kanuni za imani. Huwezi wakati huo; huwezi sasa. Kamwe hutaweza kufanya hilo.

59 Kwa hiyo, wasingeweza kuipokea, kwa kuwa waliwazia zaidi juu ya kanuni zao za imani kuliko walivyokiwazia kile Kipawa.

60 Hivyo ndivyo ilivyo siku hizi. Watu hawawezi kukubali kunena kwa lugha, kanisani mwao. Ingeiangamiza kanuni yao ya imani. Hawawezi kuukubali uponyaji wa Kiungu, ubatizo wa Roho Mtakatifu, na Mafundisho makubwa kama hayo ya

Biblia, Kweli za kimitume. Kwa nini? Kwa sababu kanuni yao ya imani inalihukumu. Loo, ni ujinga wa namna gani, kuichukua karatasi iliyokifunga hicho Kifurushi na kuitupilia mbali ile Zawadi. Kama yule punguani, yeye alikichukua kile kifurushi na kukikubali, kisha akaitupilia mbali zawadi. Hivyo ndivyo kanisa lilivyo, na watu wanavyofanya siku hizi, wanasahau ya kwamba Zawadi ya Mungu ni Uzima wa Milele kupitia kwa Yesu Kristo. Amekataliwa siku hizi kadiri alivyokataliwa wakati huo. Usiku huu wa Krismasi, Yeye amekataliwa kadiri alivyokataliwa usiku wa kwanza wa Krismasi. Hawawezi kufanya hivyo, kwa sababu haikubaliani na kanuni zao za imani. Kote katika nyakati, tumekuwa na jambo lile lile.

61 Si ajabu hapakuwapo na nafasi kwa ajili yake katika nyumba ya wageni. La. Haikuwa imefungwa vizuri; haikuwa imefungwa, kuzungushiwa makaratasi ya kiungwana. Ilikuwa imefungwa kama Zawadi, kama Zawadi kutoka kwa Mungu, iliyotumwa kutoka kwa Mungu, Mungu ambaye hawakujua chochote juu Yake. Wanadai walimjua. Na wanadai walikuwa wakimtazamia. Bali Yeye hakuja kwa njia waliyofikiria alikuwa anakuja, kulingana na kanuni zao za imani, wala wasingeweza kuipokea Zawadi ya Mungu. Alikuwa amefungwa vinginevyo. Alikuwa amevikwa kama mtoto mchanga. Alizaliwa katika hori. Alitoka kwa watu maskini. Alitoka kwenye kundi la "walokole," kwa hiyo wangewezaje kupokea kitu kama hicho? Si ajabu hapakuwapo na nafasi kwa ajili yake katika nyumba ya wageni.

62 Hakuna nafasi kwa ajili Yake bado, makanisani. Wanamfukuza. Hawaiamini. Watasema, "Ondoeni Kitu kama hicho! Ni ulokole. Hatutaki uhusiano wowote Nacho. Kinahitilafiana na mafundisho ya baba zetu, mafundisho ya kanisa hili, mafundisho ya kanuni zetu za imani za babu zetu." Kwa hiyo, Kristo amekataliwa tu leo kadiri alivyokataliwa huko nyuma. Hakuna nafasi, usiku wa leo, katika makanisa yetu mazuri, makanisa yetu makubwa, makanisa yetu mazuri. Hakuna nafasi katika jamii ya watu wa dini zetu, siku hizi, kwa ajili ya mkutano wa Roho Mtakatifu. Hawamtaki. Yeye, Yeye huwadhalilisha mbele ya matabaka ya nchini. Huwadhalilisha kuwazia kwamba wanajinyenyekeza kushuka madhabahuni, kulia na kungojea hapo mpaka wamejazwa na Nguzu zitokazo Juu, wapate kusimama watoke hapo wakiwa na upya wa Maisha; kuwafanya wanawake waachilie nywele zao zikue, na kutenda kama iwapasavyo wanawake; kuwafanya wanaume watupe sigara zao, na kuacha unywaji wao wa pombe, na kuwatendea mema familia zao. Imezidi sana kwao. Kwa hiyo wanashikilia kanuni yao ya imani, ya kanisa lao, badala ya kuipokea Zawadi ya Mungu, Zawadi ya Mungu ya Krismasi.

63 Afadhali wawe na kanuni ya imani kuliko kuwa na Zawadi, afadhali wawe na karatasi kuliko ile Zawadi. Wanataka karatasi, hakika, kitu ambacho kimepambwa sana, fujo kubwa

wanayoweza kufanya kuihusu. Lakini ile Zawadi halisi iliyo ndani yake, hawaitaki Hiyo. Mnaona?

64 Alikuwa amefungwa, basi, katika kitambaa kichafu, nguo za kitoto. Naye amefungwa, leo hii, katika kitu kile kile, ambacho wanakiita, "mtakatifu anayejibingirisha, ulokole, kundi la wazushi." Imevikwa nguo za kitoto, wala ulimwengu haumtaki. Loo! nina furaha sana kuiinua hiyo nguo. Nione kilicho chini yake: Uzima wa Milele, Mungu, aliyefanyika mwili na kukaa miongoni mwetu.

65 La, hawakumtaka. Aliharibu jamii yao ya kidini.

66 Kuipokea, leo hii, inawaingilia. Loo, kama mtu fulani angesimama kanisani, na kuanza kupaza sauti, ama kumsifu Mungu, ama mtu fulani aseme, "Amina," kama kundi hili la wahudumu hapa, kitu fulani, ama katika wasikilizaji, upesi bawabu angewaongoza mlangoni. Na kama jina lako lilikuwa kwenye kitabu, lingefutiliwa mbali upesi. Mnaona? Mungu hana na—nafasi.

67 Kama Rais mteule, Kennedy, angeutembelea mji huu hapa, bendera zinge—zingepeperushwa, na—na mapambo yangepepea, na—na mazulia yangetandikwa, na—na makaribisho makubwa sana u—usiyopata kuyaona. Ambayo, hilo ni sawa kama wakitaka kufanya hivyo. Yeye ni Rais mteule wa Marekani. Lakini kama angekuja, wange—wangefanya hayo yote, nao wangempa makaribisho yaliyo makubwa kuliko yote, na wazia, kwamba, "Yeye alijidhili apate kuja kwenye jiji lililo dogo sana kama Jeffesonville, Indiana, wakati New York pamoja na miji mikubwa inamwita, kila mahali, kwa muda kidogo tu wa wakati, kuzungumza naye." Kama angekuja Jeffersonville, kwenye mji maskini kama wetu, jinsi ambavyo wangeweka, kile tunachokiita, "mapokezi yaliyotia fora." Nao wangefanya kila kitu, na—na kuipamba mitaa, na—na kufanya kila kitu kumfanya ajisikie kukaribishwa. Hilo ni sawa, endapo wewe ni mwanasiasa. Hiyo ni sawa.

68 Lakini Yesu anaweza kuingia katika mfano wa ufufuo wa Nguvu Zake, anaweza kuingia katika Roho Mtakatifu, na anaweza kuonyesha ishara na maajabu, na kila gazeti litalikosoa. Watu wataliita "watakatifu wanaojibingirisha." Watasema, "Hao watu ni wendawazimu." Si ajabu tuna bomu la atomiki lililoandikwa jina letu juu yake. Kuikataa rehema, hakuna kilichosalia ila hukumu. Loo, hawataipokea. Wasingeipokea wakati huo. Hawataipokea sasa.

69 Kwa nini hawakuipokea? Nataka tu kuuliza, kwa nini hawakutoa, hawakuikubali Zawadi ya Mungu ya Krismasi? Kwa nini hawakupokea, hawakuipokea? Kama ni zawadi tu ambayo wangeliiangalia, Nayo ilikuwa inafaa katika shirika lao, ingalikuwa ni sawa. Kama ninii yetu . . .

70 Kama dini hii ya Roho Mtakatifu ingalienea kwenye shirika la watu siku hizi, wangeichukua. Vema, kwa nini hawaichukui, basi? Kwa sababu wanafikiria zaidi juu ya shirika lao kuliko wanavyomwazia Kristo. Hiyo ni kweli.

Mnasema, "Unazungumza kwa ukali sana kumhusu Yeye."

71 Ninamtetea. Yeye ni Bwana wangu. Nina ninii. . . Mimi—mimi—mimi ni mtumishi Wake. Nina haki ya kupiga makelele dhidi ya mambo mabaya. Hiyo ni kweli. Nao Wakristo wanaamini hilo, na wanajua hilo, na wanalikubali hilo, na wanajua ni Kweli.

72 Ni nini kilichokuwa sababu yao kutokipokea Kifurushi hiki kilichofungwa? Walijua kilichokuwa ndani Yake, wala hawakukitaka.

73 Hiyo ndiyo sababu makanisa na watu, leo hii, na serikali nchini, hawataipokea Zawadi ya Mungu ya Krismasi, ni kwa sababu wanajua kilicho ndani Yake. Hawakitaki. Kitawafanya wanawake watende tofauti. Kitawafanya wanaume watende tofauti. Itakubidi kuvumilia jina la "mlokole." Itakubidi kushika njia pamoja na wachache wa Bwana waliodharauliwa. Itakubidi kuyasafisha maisha yako. Itakubidi kuachana na uchoyo wako. Itakubidi kuacha kufanya mabaya, kudanganya, kuiba, kusema uongo, kufanya uzinzi. Itakubidi kuacha mambo haya. Wala watu hawaitaki. Ingawa huenda wanajua ni ya kweli, bali hawaitaki. Inawaletea Kweli nyingi sana. Inazifichua dhambi zao, kwa hiyo basi hawaitaki, hawataki uhusiano wowote nayo. "Msiikaribie."

74 Hivyo ndivyo ilivyokuwa katika siku zile. Walijua ni nini kilichokuwa kimefungwa ndani Yake, kwa hiyo wakasema, "Kiondoshe."

75 Hawakitaki. Ni jambo lile lile, siku hizi, kamwe hawakukitaka. Wala hawamtaki Roho Mtakatifu, siku hizi, ni kwa sababu wanajua ni kitu gani kimefungwa ndani Yake. Wanaweza kuangalia m—mtu akimpokea Roho Mtakatifu. Wanasimama huko nje na kuona kwamba mwanamke yule, labda duni awezavyo kuwa, mpaka hata mbwa watamwangalia kwa shida; na kumwona mwanamke huyo akiondoka kwenye madhabahu hayo, mtu mpya; kumwona mwanamke huyo akisafisha maisha yake, akitoka nje na kutenda kama mama wa heshima. Kumwona mmoja ambaye huzikimbilia karamu za karata, anavuta pakiti nne ama tano za sigara kwa siku, anakaa kwenye baa, mlevi wa kawaida; nao wanajua, kama kamwe wakiikubali Zawadi hii ya Mungu, imefungwa katika Kifurushi kinachoitwa Yesu Kristo, itaharibu kila sehemu ya anasa zao za kilimwengu, maana Yeye hatavumilia hilo. Inawafanyia jambo fulani, Hiyo huwabadilisha watu. Watu hawataki kubadilishwa. Wao, "Achana nami."

76 Inanikumbusha juu ya mtu yule aliyepagawa na pepo. Ambaye, Yesu aliingia Gerasi, na kulikuwako na mtu kule, alikuwa na pepo elfu mbili ndani yake. Nao wakasema, "Kwa nini usininii . . . Tuna nini Nawe? Kwa nini Wewe waja hapa? Ondoka nchini mwetu. Hatukutaki hapa." Walitaka kuachwa peke yao. Hao watu walijisikia vizuri zaidi, walijisikia nyumbani, pamoja na pepo, kuliko walivyojisikia pamoja na Yesu. Kwa hiyo walisema, "Ondoka nchini mwetu, hatukutaki huku."

77 Maskini yule Jeshi, yeye ndiye tu ambaye—ambaye alitaka usaidizi. Yeye sikuzote huja kwa wale wanaomtaka. Yeye huja kwa wale wanaomhitaji. Kwa hiyo, alikuwa ndiye pekee aliyesaidiwa. Mara nyingi nimewazia, nitakapofika Mbinguni, ninataka kuona ushuhuda wake ulikuwa na u—uzito gani juu ya wafuga nguruwe huko Gerasi. Vema, kama itawagharimu kundi la nguruwe, hawakutaka uamsho wowote.

78 Kama itawagharimu watu chochote, hawataki uhusiano wowote Nayo. Hivyo ndivyo ilivyo siku hizi, kama itakugharimu karamu zako za karata, nyakati za anasa, sigara zako, dhihaka zako chafu, uchafu wote na kadhalika wa ulimwengu. Sababu ya wao kutoitaka, itawagharimu kitu fulani, jina lako kubwa la jamii pamoja na kumetameta kwake kwingi.

79 Lakini itakupa jina lililoandikwa katika Kitabu cha Uzima cha Mwana-Kondoo, kisichopauka. Kwa hiyo, jichagulie. Wewe ni mtu mwenye hiari ya kujichagulia. Loo! pokea Zawadi ya Mungu ya Krismasi, ndilo ombi la—langu kwako. Naam.

80 Hawaitaki, kwa sababu inafanya jambo fulani kwao. Ama, na serikali je? Serikali haikumtaka. Herode hakumtaka. La, bwana. Kwa sababu gani? Angeibadilisha ratiba yake.

81 Wala serikali haimtaki, siku hizi. Tunadhaniwa kuwa ni taifa la Kikristo.

82 Mbona, UN hawamtaki. Watachukua kila wazo lingine ulimwenguni kando na Lake. Kamwe hawataomba dua. Hakuna maombi kwenye vikao hivyo. Wanaingia tu mle na "kushambuliana kinyang'au," kama msemo wa kale ulivyo wa kutoka mitaani. Hawamtaki Kristo. Ingembidi kubadilisha mipango yao, kwa hiyo hawamtaki. Hawakumtaka wakati huo. Hawamtaki sasa.

83 Makanisa hayakumtaka, kwa sababu hakukubaliana na kanuni zao za imani. Aliwaambia kwamba walikuwa, kasema, "Enyi kizazi cha majoka, enyi kuta zilizopakwa chokaa." Aliwaita kila kitu kingaliweza kufunzwa. Akamwambia maskini Herode, kasema, "Nenda kamwambie huyo mbweha." Basi ni kitu gani kilicho kichafu kuliko mbweha? Ni kitu gani kinachovunda na kilicho duni kuliko maskini mbweha mchafu? Yesu alisema, "Hivyo ndivyo alivyo." Kwa hiyo, Yeye—Yeye—Yeye

aliita cheusi "cheusi," na cheupe "cheupe." Yeye—Yeye—Yeye aliita kosa "kosa," na kweli "kweli." Kwa hiyo, hawakutaka hilo.

84 Makanisa siku hizi hayataki mchungaji aliyejazwa na Roho Mtakatifu, ambaye kweli atalichemsha kabisa, na kukwambia lililo kweli na lililo uongo. Hawaitaki. Wangemfukuza, upesi sana. Halmashauri ya mashemasi ikutane na kumfukuza, wamlete mwingine, na kuzungumza juu ya kanuni zao za imani.

85 Ndugu, sijui kanuni yoyote ya imani ila Kristo, hakuna sheria yoyote ila upendo, wala kitabu chochote ila Biblia. Hiyo ndiyo tunayohitaji. Hiyo ndiyo makanisa yanayohitaji.

86 Lakini ha—ha—hao watu hawaitaki. Kwa hiyo, wamelifunganisha kanisa sana kwenye madhehebu haya mpaka wanaweza wakaichukua halmashauri ya wadhamini na kumgeuza mchungaji mzuri kwa njia yoyote watakayo. Ila hawawezi kumgeuza Mungu, hilo ni jambo moja hakika. Mungu atabaki Mungu. Hawatamkaribisha. Wanawakaribisha ma—marafiki zao na wanasiasa wao, na kadhalika, bali hawatamkaribisha Kristo.

87 Afadhali wawe na Baba Krismasi, wakati wowote. Ulimwengu umechukua mamlaka. Baba Krismasi amechukua mamlaka. Vema, mwajua, watoto wadogo hata hawajui tena maana ya Krismasi.

88 Hawajui maana ya Pasaka, ni—ni kisungura cha Pasaka, namna fulani ya sungura, ama maskini kuku aliyepakwa rangi ya manjano, ama kitu fulani. Mungu, ufufuo, una uhusiano gani na kuku, ndege mchafu sana aliyeko? Ni kitu gani kilicho kichafu zaidi kuliko kuku? Nao wa—wanamweka mle ndani, na kupachukua mahali pa Kristo.

89 Ni kitu gani kilicho cha uwongo kuliko Baba Krismasi? Hapajawahi kuwa na kitu kama hicho. Kuwaambia watoto uongo, utawajibika kwake kwenye Siku ya Hukumu.

90 Si ajabu watu hawajui la kufanya. Wao ni. . .Wao—wao hawataki kabisa jambo lililo halisi. Watachukua kitu chochote bandia, bali hawataki kitu kilicho halisi. Hawazitaki zawadi za Mungu. Loo, jamani! Bila shaka. Hawamtaki Yesu, hilo ni jambo moja.

91 Nimeandika hapa, sababu moja hawakumtaka, ni kwa sababu kwamba wakati alipoingia hekaluni mwao, na kuona uchafu wao hekaluni, alizipindua meza na kuwafukuza wabadilisha fedha. Akalisafisha.

92 Na kama kamwe wangemruhusu Roho Mtakatifu kuingia katika moja ya makanisa haya makubwa hapa, Yeye angelisafisha. Kwa hiyo, hawawezi kuikubali, mnaona. Ingewafanya waache kucheza karata, iwafanye waachane na karamu za roki.

93 Kuweka picha zao gazetini, kama wapinga maadili, kama vile mhubiri wa Kimethodisti alivyofanya hapa chini kwenye Bustani ya Howard, Clarksville. Ninaye ndugu anayeketi hapa sasa, kama hakumchanua nywele. Mtu yeyote, mtumishi wa Mungu, anayeiweka picha yake kwenye gazeti, ana karamu ya kukiuka maadili kanisani. John Wesley angalijua hilo, angalipinduka kaburini mwake. Kwa nini? Walimkataa Kristo ambaye John Wesley alimjua, kweli, na kumkubali mkiuka maadili. Wanayo dini ya kukiuka maadili. Wana watoto wakiuka maadili, baba mkiuka maadili, mama mkiuka maadili, Rais mkiuka maadili, na kuendelea tu mbele zaidi na zaidi, na kwa hiyo inazidi tu kwenda. Loo, ni fedheha jinsi gani! Kwa nini? Wanakataa kilicho halisi.

94 Mungu alisema atawapa nguvu za upotevu, wauamini uongo wapate kuhukumiwa kwao. Mungu alisema ingefanya hivyo. Ukiikataa kweli, inakubidi kuuchukua uongo. Hakuna njia nyingine. Ukikataa kwenda kulia, huna budi kwenda kushoto, utapitia njia nyingine mbali na ya kulia. Kwa hiyo, huwezi kwenda vizuri na vibaya wakati uo huo. Wanapomkataa Roho Mtakatifu, wanamkataa Kristo, wanaukataa mpango wa Mungu, wanamkataa mjumbe, wanakataa kila kitu. Kwa hiyo, basi, wanaachwa katika dhambi zao. Hakuna kilichosalia basi ila hukumu. Ndugu Ben, hiyo ni kweli. Ninii tu, hiyo ni kweli kabisa, wao wame—wamemkataa Kristo. Wameukataa mpango Wake. Walimkataa Roho Wake. Yeye amejaribu, kwa miaka hamsini, ambayo Roho Mtakatifu amekuwa akishuka Marekani. Wamemkataa, kwa muda wa miaka hamsini. Na usiku wa leo ni nyeusi na yenye giza kuliko ilivyowahi kuwa.

95 Na hata juu ya wale aliowashukia, hapo mwanzo, watoto wao wamejiundia mashirika na madhehebu, na kuishia katika madhehebu, hata wanamkataa Mungu yeye yule baba zao walimpokea. Amina. Halafu, wanadai ni "wapentekoste." Loo, la. Haimfanyi nguruwe jike kuwa farasi, kuishi katika kibanda. La, hasha. Si zaidi ya inavyofanya Mkristo kutoka kwa mtu aliye mfuasi wa kanisa la Kipentekoste, Baptisti, Presbiteri, chochote kingine. Yeye angali ni mwenye dhambi mpaka atakapoongoka. Basi anapoongoka, yeye amezaliwa mara ya pili, Roho wa Mungu, na kubadilishwa. Naye amemkubali Kristo, naye Roho Mtakatifu ameingia ndani na kumfanya kiumbe kipya, uumbaji mpya.

96 Basi, waliikataa wakati ule. Wanaikataa leo. Yeye angezipindua meza zao za fedha. Angeipindua halmashauri yao ya wadhamini, halmashauri ya mchungaji wa—wao. Wao—wao wasingeikubali, Yeye angeninii . . . Wangepata halmashauri, vema. Loo, kungekuwako na tofauti ya jinsi gani kama Yeye aliingia makanisani leo hii, bali hawezi kuingia.

97 Tulimpata Yeye, hivi majuzi usiku, katika wakati huu wa kanisa, ametupwa nje na kanisa Lake Mwenyewe; amesimama

mlangoni, akibisha, akijaribu kurudi ndani tena. Baba mwenye rehema! Baada ya kufukuzwa, na watu Wake Mwenyewe, akijaribu kurudi kanisani Mwake tena! Yeye alisema, "Mimi Ndimi nitembeaye katikati ya Vinara vya taa Saba vya Dhahabu." Na kwenye wakati wa mwisho wa kanisa, Yeye huyu hapa, nje. Walimfukuza. Wapi? Katika wakati huu wa Laodikia. Akisimama tena, akijaribu kurudi ndani tena, kwenye mlango Wake Mwenyewe, kwa kanisa Lake Mwenyewe. Ni jambo la kusikitisha jinsi gani! Hiyo ndiyo moja ya picha za kusikitisha sana ambazo Biblia inachora, ni mlango huo wa pili wa Ufunuo, wa 3, hasa, jinsi ambavyo kwamba, Kristo amefukuzwa!

98 Kuna jambo lingine la kusikitisha. Nafikiri moja ya Maneno ya kusikitisha sana aliyopata kusema Yesu, yalikuwa ni wakati aliposema, "Baba, ninajitakasa Mwenyewe, wapate kutakasika." Kwa maneno mengine, Yeye alikuwa na haki. Alikuwa ni mwanadamu. Alikuwa na haki ya makazi. Alikuwa na haki ya kuwa na familia. Alikuwa ni mwanamume, mwanamume kama ulivyo wewe, ama nilivyo mimi, mwanadamu katika uanaume Wake kadiri tulivyokuwa. Alikuwa na haki kwake. Lakini Yeye alikuwa akiwafunza wanaume kumi na wawili waliokuwa wataieneza Injili kote ulimwenguni, kwa hiyo alijitakasa Mwenyewe kwa ajili yao. "Najitakasa Mwenyewe, kwa ajili yao." Zawadi ya Mungu, akiendelea kujitakasa Mwenyewe.

99 Loo, enyi zawadi za Mungu, ninyi watu mnaodai ya kwamba mmempokea Roho Wake, endeleeni kujitakasa. Naam. Kaeni mbali na mambo ya ulimwengu, jitakaseni. Loo!

100 Ni nani alijua kile kilichokuwa kwenye Kifurushi hiki cha Zawadi? Kuna mtu yeyote aliyepata kujua kile kilichokuwa ndani Yake? Nina furaha sana kwamba kulikuwako. Ni nani aliyeijua? Kilikuwa ni Kitu kilichofichwa, Jiwe lililokataliwa, bali kulikuwako na mtu aliyepata kujua kilichokuwa ndani Yake. Nina furaha sana.

101 Ninapenda kuchunguza mambo, nanyi je? Ninapenda kuchimbua vibamba na kuvipiga msasa kwelikweli, nione kile—kile kilicho ndani yavyo, nikiweke mbele ya Geiger.

102 Aliwekwa mbele ya Geiger, pia, pale Kalvari. Alikuwa asilimia mia moja. Hakika. Alikuwa ndiye Dhahabu kuu kuliko yote waliyowahi kuipata, Almasi ya bei kubwa kuliko zote iliyo—iliyopata kuwapo. Bi—Biblia ilisema, "Ufalme wa Mbinguni ni kama mtu anayenunua almasi. Basi alipopata Hii iliyo kuu, aliuza zingine zake zote, na kuilipia tu, kuinunua Hiyo." Yeye ndiye Almasi kuu sana iliyokaratiwa iliyowahi kutolewa kwenye mavumbi ya ardhini, Dhahabu kuu kuliko yote iliyowahi kutolewa mavumbini. Yeye ni Kito, Kito cha Mbinguni, Almasi kubwa.

103 Wakati almasi kubwa inapopatikana Afrika Kusini. Nimepitia kwenye i—ile migodi mikubwa ya almasi huko

Kimberly. Nao wanazichukua almasi hizo, ndipo wanapozitoa mavumbini, mbichi, basi wanazichonga. Na sababu ya kuzichonga, kuzikata, ni kuakisi nuru. Kutoa nuru kwake, karati ya hizo, ikionyesha karati zilizo ndani ya almasi hiyo. Kama haina moto mwingi na kumetameta, si almasi nzuri, bali inapokuwa . . . ni kioo; bali wakati ni almasi halisi, almasi halisi iliyokaratiwa, itaakisi na kuonyesha rangi mbalimbali.

104 Hivyo ndivyo Yeye alivyokuwa. Alikuwa ni Almasi. "Naye alijeruhiwa kwa makosa yetu. Alichubuliwa kwa uovu wetu. Adhabu ya amani yetu ilikuwa juu Yake, na kwa mapigo Yake sisi tuliponywa." Loo, hiyo miale ya upendo wa Mungu na Nuru inaakisi kutoka Kwake: Nguvu za uponyaji, upendo, ufufuo. Mungu alimjeruhi, na kumchubua, na kumkatakata, na kumkata, kwa upanga wa Kirumi na—na—mjeledi wa Kirumi, mpaka mbavu Zake zikapasuka. Nayo Damu ikitiririka kutoka mgongoni Mwake, na juu ya kichwa Chake, na kupitia ndevu Zake, na kutoka miguuni Mwake. Loo! Alikuwa akifanya nini? Alikuwa akiakisi upendo. Akaukumbatia msalaba! Badala ya foronya nyororo, ya manyoya; hori la mabua. Badala ya maskini joho dogo la waridi, la kuvalia; nguo za kitoto.

105 Loo, ndugu, unaweza kuona kilindi cha upendo ni nini? Nilikuwa nikizungumza, baadhi ya watu nyumbani mwangu, hivi majuzi usiku. Hakuna mtu angaliweza kuchezea jinsi upendo wa Mungu ulivyo na kilindi. Ule "Loo, upendo wa Mungu, jinsi ulivyo mwingi, jinsi ulivyo safi!" Kifungu hicho cha mwisho, ama, kifungu cha kwanza, ninaamini ndicho, kilipatikana kwenye ukuta wa hospitali ya wendawazimu:

> . . . kwa, sisi kwa wino kuijaza bahari,
> Na kama mbingu zilifanyizwa kwa karatasi;
> Kila kikonyo duniani kiwe ni unyoya wa
> kuandikia,
> Na kila mwanadamu kazi yake iwe ni uandishi;
> Kuandika upendo wa Mungu aliye juu
> Kungeikausha bahari;
> Ama kweli gombo lingeweza kuchukua yote,
> Hata likitandazwa anga hata anga?

106 Wazia vikonyo ambavyo vimekuwa duniani, vikifanya manyoya ya kuandikia. Na mabilioni ya watu, kazi yao ni uandishi. Kuandika herufi tano ndogo, u-p-e-n-d-o, ninamaanisha herufi nne ndogo, "upendo," [Kiingereza: "l-o-v-e."—Mfa.] upendo wa Mungu, kungeikausha bahari. Wakati, sehemu nne kwa tano za dunia ni maji. Nami nilisimama huko, Mlima Palomar, na kuangalia kwa ile darubini, unaweza kuona maili milioni mia moja ishirini za anga ya nuru. Ama gombo lingeweza kuchukua yote, ingawa limetandazwa anga hata anga?

107 Upendo wa Mungu. Jinsi Mungu alivyojifunua Mwenyewe, kisha akaja, Kifurushi cha Krismasi, akalazwa kwenye ubua. Kitu cha kwanza alichokuwa nacho, kilichokifinya kichwa chake kidogo, kilikuwa ni ubua, na kipande kichafu cha nguo ya kitoto alichofunikwa. Kitu cha mwisho alichokuwa nacho kilikuwa ni taji ya miiba, huku kitambaa kichafu kimezungushiwa machoni Mwake; na kupigwa kichwani, wakisema, "Kama Wewe ni nabii, tuambie ni nani aliyekupiga," kisha akaangikwa msalabani. Upendo, ukiwafikia! Wakati watoto Wake Mwenyewe wakililia Damu Yake, Yeye alipaza sauti, "Baba, wasamehe, hata hawajui wafanyalo." Huo ndio upendo.

108 Kanisa haliutaki Huo. Wanataka kanuni ya imani. Tunahitaji upendo. Kanisa linakufa, kwa kanuni za imani. Linaweza tu kuishi kwa upendo, kwa sababu upendo ni Uzima wa Milele. Upendo hushinda mambo yote. Upendo ndio nguvu kuu kuliko zote iliyopo. La, hawakumtaka, kwa sababu wanajua kilichokuwa ndani ya hiyo Zawadi.

109 Lakini baadhi yao walifunuliwa, kile—kile Zawadi hii ilichokuwa, kilichokuwa ndani Yake. Baadhi yao waliangalia ndani Yake. Ninaamini, wa kwanza kuangalia ndani ya Kifurushi hicho cha Krismasi, mwajua alikuwa ni nani? Ninaamini, walikuwa ni Malaika. Malaika walijua. Ilifunuliwa kwao. Waliijua, kwa sababu walikuja ubavuni mwa kilima.

110 Labda, maskini Mariamu ameketi kule juu, amechoka, amejaa mavumbi. Maskini mvulana mchungaji akapitia pale, akinuka kama kondoo, akamwona maskini mama huyo ameketi pale, usiku huo, ukimaanisha jambo fulani. Kama tu vile watu siku hizi wanavyoweza kuona ya kwamba kuna kitu kinachokaribia kutukia. Wakati mzuri sana, watu hawajui wageukie wapi. Labda maskini mvulana mchungaji alipitia pale na kumwona maskini mama huyo. Kitu fulani kikamgusa. Akasema, "Nina maji baridi hapa kwenye chupa hii. Ungetaka kunywa kidogo?" Ndipo maskini familia hiyo ikamshukuru, maskini mja mzito akiyanywa hayo maji.

111 Labda huyo alikuwa ni mmoja wa maskini wachungaji waliokaa kule kilimani usiku huo, akiwa huko chini zizini, ambako Mtoto mchanga alikuwa akilia. Loo, basi, ulimwengu, hapakuwapo na nafasi kwa ajili Yake. Hakuna mtu aliyemtaka. Lakini wakati uo huo, mchungaji huko nje kilimani, Malaika walishuka wakaanza kuimba noeli ya kwanza, "Leo hii, katika mji wa Daudi, amezaliwa kwenu, Kristo Mwokozi." Ilifunuliwa.

112 Hiyo ndiyo njia pekee mtu yeyote ulimwenguni atapata kujua kile kilicho kwenye Kifurushi hicho. Haina budi kufunuliwa kwako. Utaikataa, useme ni—ni ulokole; lakini unapopata ufunuo, utaitafuta. Utafunguka. Naye Mungu ataingia na kula pamoja nawe, nawe pamoja Naye, wakati

ukiwa tayari kufungua mlango, kumwacha aingie. Maskini Kifurushi hicho kidogo kinachoubisha moyo wako, Zawadi kubwa sana ya Krismasi iliyowahi kutolewa, ya kwanza na iliyo kuu kuliko zote. Kifurushi hicho kidogo, kinachoubisha moyo wa mwanadamu, "Nitaingia na kula." Kamwe hutaijua mpaka itakapofunuliwa kwako. Inapofunuliwa kwako, ndipo utaanza kuitafuta.

113 Unapoona kwamba Hiyo ni Uzima, na njia pekee ya Uzima, wakati unapoona ya kwamba kanisa lako limekauka na limekufa, wakati unapoona ya kwamba ku—kupeana kwako mkono na mchungaji, ama unanyunyiza kwa kijichupa cha chumvi, havina uhusiano wowote na Hiyo, basi utaanza kuchunguza.

114 Wakati unapolala kitandani, ukifa, naye daktari anasema, "Hakuna chochote kilichosalia kwako. Utakufa katika dakika chache." Utataka kuangalia kwenye Kifurushi hicho basi. Kiangalie, usiku wa leo, maana kitaondolewa kwako wakati huo. Biblia ilisema, "Ukinikataa Mimi katika siku za afya yako, kama ulivyo sasa; wakati maafa yatakapokuja, nitakucheka tu." Kwa hiyo afadhali ukichunguze hicho Kifurushi usiku wa leo.

115 Yote haya yanahusu nini? Nuru, Nuru takatifu zikija kutoka Mbinguni, zikipigwa picha, ishara kuu, utambuzi, nguvu, kunena kwa lugha, kufasiri, kusema mambo yanayokuja, nguvu za Injili, kuwaponya wagonjwa, kuzichukua kansa na kuziponya, macho mapofu kufunguka, mambo yote ya namna hii. Yote yanahusu nini?

116 "Mbona, ni kundi la watakatifu wanaojibingirisha." Kuwa mwangalifu! Hiyo ni nguo ya kitoto, huenda ikawa.

117 Vivyo hivyo na Balaamu. Yeye aliwaziaje ya kwamba Mungu asingewalaani watu kama Israeli? Lakini alishindwa kuona. Yeye aliiangalia ile nguo ya kitoto, badala ya kuona ule Mwamba uliopigwa pamoja na ile Nyoka ya Shaba iliyokuwa ikiwatangulia, kufanya upatanisho.

118 Ndivyo ilivyo siku hizi, badala ya kuziona Nguvu za Roho Mtakatifu zikifanya ishara Zake za Masihi, na maajabu miongoni mwa watu, kama Yeye alivyoahidi angefanya katika siku za mwisho. Kama Yeye alivyosema, "Kama ilivyokuwa katika siku za Lutu, ndivyo itakavyokuwa katika kuja kwa Mwana wa Adamu," wakati atakapoanza kufanya ishara hizo na maajabu miongoni mwa watu, akijionyesha Mwenyewe kuwa yu hai. Ni kitu gani? Miongoni mwa watu maskini na wanyenyekevu, maskini.

Wataiita "ulokole," waitupe nje. Afadhali uchunguze kabla haijakuacha kwa mbali sana. Naam.

119 Wachungaji hawa wanaonuka, ingekuwa vigumu kwa watu kuwaruhusu wawakaribie. Walikaa huko nje na kulala pamoja na kondoo hao, na kwenye godoro lile lile la majani makavu

walimolala, na mahali pale pale, hasa, na—na wakawachunga hao mpaka, wao, ungeweza kusikia harufu yao kama tu kondoo wanaokuja.

120 Mtu yeyote anajua ya kwamba mchungaji anayewachunga kondoo, yeye hulala papo hapo mlangoni pamoja na hao kondoo, analala moja kwa moja miongoni mwao. Yesu alisema, "Mimi ndimi mlango wa zizi la kondoo." Mara nyingi nilishangaa hilo liliwezekanaje, mpaka nilipoenda kwenye Nchi Takatifu. . . ama Mashariki, hasa. Ndipo nikakuta jinsi mchungaji anavyowaingiza kondoo ndani, kisha analala chini, mlangoni. Kondoo hawezi kutoka nje pasipo kumruka. Mbwa mwitu hawezi kuingia pasipo kumruka. Yeye ndiye mlango.

121 Nina furaha ya kwamba Yesu alilala mlangoni mwa moyo wetu. Hatuwezi kutoka, wala kufanya lolote, pasipo Yeye kujua, wala hakuna kitu kinachoweza kuingia pasipo Yeye kujua. Kwa hiyo Yeye atafanya kila kitu kifanye kazi pamoja kwa manufaa ya wale wampendao. Linapaswa kutufanya kulia na kupaza sauti, na kumsifu Mungu, na kusema, "Mungu ashukuriwe kwa ajili ya Mwokozi, M—M—Mchungaji ambaye atalala mlangoni mwa moyo wetu, na kutuonya wakati kitu chochote kinapokuja, awe tayari kukikabili." Naam.

122 Huko mbali nchini kulikuwako na watu wanyenyekevu, wenye hekima. Waliitwa Mamajusi, "watazama nyota." Nilipokuwa huko Mashariki, sio muda mrefu uliopita, wangali wanaketi vile vile. Wao ni watu maskini sana. Wanatembea watatu watatu. Wanaketi moja kwa moja mtaani. Mimi pamoja na Billy, huko India. Huko nyuma ndani kabisa wanakotoka, India. Sasa, wao walisema, "Tumeiona Nyota Yake Mashariki." Walikuwa Mashariki wakati walipoiona hiyo Nyota. Yerusalemu iko magharibi, kwa hiyo Palestina ilikuwa magharibi mwa—mwa India. Kwa hiyo waliiona Nyota Yake wakati wakiwa Mashariki, ndipo wakaja kumwabudu.

123 Sasa, hawa Mamajusi, kamwe hawakuketi chini ardhini. Wanachuchumaa tu chini. Nao wanaketi pale siku nzima. Usiku, wana mnara mkubwa. Wanapanda huko juu na kukaa kwenye mnara huu. Wanawasha mioto, na kuzungumza kuhusu nchi, kuanguka kwa falme, na—na kudhoofika kwa milki. Na wao—wao wanamwabudu Mungu mmoja wa kweli. Hiyo ni kweli. Wao ni—wao ni waaminio. Wao ni Waislamu. Kweli, walitokana na Wamedi na Waajemi, huko nyuma kabisa katika siku za Danieli. Nao hao ndio. . .

124 Naye Petro alisema, katika Matendo 10:35, ya kwamba "aliona kwamba Mungu hana upendeleo wa mtu wala taifa, bali Yeye. . . wote katika kila taifa wamchao," na mtu yeyote atakayemcha Mungu. Hebu waangalieni hao Mamajusi huko, wakiiona ile Nyota Zawadi ya Mungu, na kuitambua kabla

makuhani hekaluni huko Yerusalemu, miongoni mwa watu wa kidini. Naam, bwana. Amina.

125 Mamajusi, ninaweza kuwaona wameketi pande zote za huo moto mtakatifu, usiku mmoja. (Hivi tuna muda mfupi tu? Naam.) Wameketi kuuzunguka moto huo mtakatifu, wakizungumza, kisha wangepanda juu. Loo, walizichunguza sayari za angani. Walizifahamu zote vizuri. Kila msogeo, walijua habari zake. Kwa hiyo usiku mmoja, wakiwa wameketi pale, labda wakiimba nyimbo, nao wangepanda juu ya kitu hiki kikuu, na kuchunguza. Walijua kila nyota, mahali ilipokaa. Waliijua kwa jina, maana walizichunguza sayari za angani. Na si ajabu kwamba Mgeni huyo miongoni mwa hizo sayari za angani aliwachangamsha. "Vema," wakashangaa, "Jamaa huyu mpya hapa juu ni nani?" Loo, jamani! "Kuna jambo jipya limetukia, ni la kimbinguni." Hilo, lilielekeza wapi? Kurejea kwenye Maandiko.

126 Sasa, walijua kuhusu Maandiko, maana Danieli alikuwa ndiye kiongozi wao. Mnajua hilo; mlango wa pili wa Danieli, unatwambia ya kwamba yeye alifanywa kiongozi wao, kwa hiyo aliwafundisha. Hapana shaka, usiku mmoja, walikuwa wameketi pale, wakisoma katika Maandiko, kuhusu, "Naye Danieli alisema 'niliangalia falme hizi zote,' mpaka hatimaye zikawa vile zilivyokuwa, kila moja, Wamedi na Waajemi na kuendelea hata ikafikia kwenye Rumi. Ndipo basi hatimaye 'akaona Jiwe lililokatwa mlimani, pasipo kazi ya mikono.'" Nao wakasema, "Hapana shaka wakati huo umewadia." Ndipo wakakumbuka marudio ya huko nyuma kabisa, kabla ya wakati huo, huko nyuma katika siku za safari ya—ya Israeli, wakati walipokuja na kumsikia Balaamu akisema, wakati alipowaona Israeli, yeye alisema, "Itazuka Nyota kutoka kwa Yakobo." Amina. Hapana shaka ilikuwa ni yapata wakati huo, wakati walipokuwa wakiwazia mambo hayo, ambapo yule Mgeni mpya alijitokeza.

127 Kwa kawaida ni wakati unapoiweka nia yako juu ya Kristo ndipo Yeye anapokuja kwako. Kwa kawaida—kwa kawaida kwenye nyakati ambapo unawazia kumhusu Yeye, ndipo Yeye anapojitokeza. Mwajua, wakati unapowazia kuhusu kuwa sawa, kufanya mema, hapo ndipo Yeye anapokujia, kukusaidia.

128 Na hapana shaka ilikuwa ni yapata wakati huo, na wao—wao hapana shaka waliangalia juu na kumwona Mgeni huyu mpya. Ilianza kuwaongoza kuelekea Magharibi. Upesi wakaanza kwenda magharibi, wakishuka chini kuuvuka mto Tigri, wakashuka kupitia jangwani, wakapanda kupitia milima, wakashuka kupitia matopeni, loo, jamani, wakaendelea mbele zaidi, zaidi. Walijua ya kwamba jambo fulani lilikuwa likitukia, jambo fulani la kimbinguni lilikuwa limetukia.

129 Nao walifika wapi? Walisema, "Hakika, kama huu ni unabii wa Danieli, huo mji mkuu wa Yerusalemu, huo mji mkuu wa

watu wa kidini wa taifa hilo wote watakuwa tayari kumpokea Mfalme wao. Watajua yote yanahusu nini, tutakapofika kule. Sisi hatufahamu, sisi wenyewe, hata hivyo. Sisi ni Mamajusi tu, watu maskini, wanyenyekevu. Lakini, tumekuwa tukitazamia kitu fulani, nasi tunaona kitu fulani kikiinuka miongoni mwetu, ambacho kidogo ni cha kimbinguni." Loo, jamani! Walikuwa tayari. Haleluya! Wakatoka, watu wanyenyekevu, kumtafuta Nyota-Mjumbe wa Mungu. Walikuwa wakitaka kumfuata Nyota-Mjumbe wa Mungu mpaka watakapoifikia ile Nuru kamilifu. Loo!

130 Ufunuo, 20, Ufunuo 1:20, ilisema hivyo, "Nyota za haya makanisa." Jambo litupasalo kufanya leo hii ni kuipata hiyo Nyota Nuru, amina, inayouakisi Utukufu Wake. Inayoziakisi Nguvu Zake. Inayouakisi Uungu Wake. Na tuifuate hiyo mpaka tutakapoipata ile Nuru kamilifu. "Endelea kuongoza magharibi, tuzidi kusonga mbele. Tuongoze kwenye hiyo Nuru kamilifu." Loo, endeleeni kusonga mbele, haidhuru itagharimu nini; kupanda milima, kushuka kupitia misituni, kila mahali pengine.

131 Basi hatimaye wakawasili Yerusalemu. Ndipo mara walipofika kwenye kanisa hili kuu la kimadhehebu, ile Nyota ikawaacha. Ajabu hii. Wakawazia, "Hapana shaka ni hapa." Kwa hiyo, huku na huku kwenye hiyo miji, wakaenda, wakiimba, wakipiga mayowe, katika kila kichochoro, kote kupitia mitaani. "Yuko wapi, Yeye aliyezaliwa Mfalme wa Wayahudi? Tumeona Nyota Yake Mashariki, nasi tumekuja kumwabudu. Yuko wapi?"

132 Ajabu, hawakuwa na jibu, moja kwa moja miongoni mwa jamii zao. Loo, jamani! Karibu ningeweza kunena kwa lugha sasa. Hawakuwa na jibu. Hawakuwa na jibu wakati huo. Hawanalo sasa. Hawajui. Wale mamajusi hawakumpata Yesu katika jamii ya dini yao. Alimpata nje ya jamii ya dini yao. Nao watu wenye hekima siku hizi, wenye hekima moyoni, hawaipati katika haya madhehebu makubwa. Hawajui lolote kuihusu. Hawana jibu. "Uponyaji huu wote wa Kiungu ni nini, unaoendelea?" wanasema. "Haya yote yanahusu nini, lugha, na tafsiri, na unabii, na *hii*, ninii...ishara za Masihi? Loo, Huo ni upuuzi. Hakuna kitu Hapo. Msininii...Hakuna kitu Hapo." Mnaona? Hawana jibu. Hawakuwa nalo wakati ule. Hawana sasa.

133 Lakini lilifanya jambo moja, Liliwafanya waanze kutafuta. Ninafikiri Ndugu yetu duPlessis kidogo amelichukua hilo sasa hivi.

134 Wakarudi. Wanawali waliolala wakarudi wakanunue Mafuta kidogo. Lakini hapo ndipo Yeye alipokuja, wakati walipoondoka kwenda kuyatafuta. Kwa hiyo tuko karibu jinsi gani sasa, wakati tunapoyaona makanisa haya makubwa yakirudi, yakisema, "Vema, huenda ikawa tumeacha kitu fulani. Afadhali tukitafute"? Kamwe hawatakipata. Kumbukeni

tu hilo. Kamwe, kamwe hawatakipata. Yamekufa. Nayo yamekufa, na kufa, na ni hivyo tu. Kamwe hayataufikia Uzima. Kumbukeni tu, nanena katika Jina la Bwana. Na Huu uko kwenye kanda. Naam, bwana. Kamwe, kamwe hawataufikia Uzima. Wamekwisha. Kwa hiyo hiyo ndiyo sababu sivutiwi na mipango hiyo. Ninavutiwa na jambo moja, kukemea kwa nguvu niwezavyo, kwa "yeyote atakaye." Sio kulifufua dhehebu, bali kumrudisha Yesu Kristo. Naam, bwana. Si katika dhehebu kamwe! Linampinga Mungu; sikuzote limempinga, sikuzote litampinga; humfungia Mungu nje, linakataa kila kitu kilichopo ambacho ni cha kiungu. Kamwe, kamwe halitaufikia Uzima. Kwa hiyo, si tofauti Krismasi hii, ilikuwa hivyo Krismasi ya kwanza. Ni jambo lile lile. Hao Mamajusi wakienda huku na huku mjini, "Yuko wapi? Yuko wapi?" Loo, jamani!

135 Hebu nikome tu hapa kwa dakika moja. Ninayo sinema. Sinayo hapa sasa. Daktari fulani anayo, Daktari Dilly, da—da—daktari mwanamke aliyeponywa katika mkutano wangu. Naye anayo hiyo kanda sasa, inayoitwa *Dakika Tatu Ifike Usiku Wa Manane,* na wakati tulipowapata hao Wayahudi wakija kwenye taifa lao kule sasa, sasa hivi katika Palestina, ambalo lilinenwa na Bwana, ya kwamba wangefanya hivyo. Kabla ya Kuja Kwake mara ya pili, wangefanya hivyo.

136 Ndugu fulani hapa, hivi majuzi, akienda Israeli, aliuliza swali, "Ninaweza kwenda huko?" Nao wakamkataza. Israeli itakuja kama taifa, sio mtu binafsi. "Taifa litazaliwa." Itakuja kama taifa.

137 Lakini, angalieni, maskini Wayahudi hao huko chini kabisa katika Iran na mahali mbalimbali. Mmelisoma katika gazeti la *Life*. Hawakutaka kuingia kwenye hizo ndege. Kamwe hawakuwa wameona moja. Walikuwa wakilima kwa maskini plau za mbao na kadhalika. Wakasema. . .Mbona, rabi alijitokeza huko nje, na kusema, "Ngojeni kidogo. Hivi nabii wetu hakutwambia, ya kwamba, tuliporudi kwenye nchi ya uenyeji wetu, tungerudi 'juu ya mabawa ya tai'?" Loo, jamani! Loo! Nao wakaja na wakaingia kwenye ndege za TWA, wakatwaliwa juu.

138 Huyo nabii hakujua ya kwamba ziliendeshwa kwa mota. Zilionekana tu kama tai wakubwa, nazo ziliruka hewani kama tai, kwa hiyo huyo nabii alisema, "Mtakaporudi. . ." Hiyo ilikuwa ni miaka elfu mbili mia tano iliyopita. Ee Mungu! Miaka elfu mbili mia tano iliyopita, wakati walipochukuliwa mateka na Warumi, na kutawanywa kwenye pepo za ulimwengu. Yeye alisema, "Wataninii. . .Sitawasahau. Nitawarudisha tena. Lakini nitayapofusha macho yao, kusudi, Wamataifa, ninaweza kuchukua watu kutoka huko, kwa ajili ya Jina Langu, niweke Jina Langu juu yao. Siku hiyo itakapokwisha, nitawakusanya tena. Nao watakaporudi nyumbani kwao, watakuja juu ya vitu

vya namna hii." Naye Isaya aliwaona wakiamka, wakija. Yeye akasema, "Juu ya mabawa ya tai."

139 Maskini rabi huyo mzee alisimama kule nje, na kusema, "Nabii wetu alisema ya kwamba tutaenda nyumbani, wakati wa mwisho, 'juu ya mabawa ya tai.'" Wakapanda ndege.

140 Ndipo waliposhuka kule, wakiwabeba walio wakongwe, vipofu na walemavu, mabegani mwao, wakiwatembeza, walihojiana nao. Ninayo moja kwa moja kwenye kanda. Kasema, "Hivi mmekuja nyumbani, kwenye nchi ya uenyeji wenu, mpate kufa hapa kwenye nchi ya uenyeji?"

Kasema, "La. Tumekuja kumwona Masihi."

141 Loo, ndugu, kuna shida gani? Wala kanisa lao halina jibu. Kuna shida gani? Tuko katika wakati wa mwisho, ndugu, wakati Nuru za jioni zinapoangaza, Nguvu za Roho Mtakatifu zimerudi Kanisani tena, kama vile zilivyokuwa hapo mwanzo. Nabii alisema, "Itakuwa Nuru wakati wa jioni." Kanisa halijui ni kwa nini wanakusanyika kule. Hawana jibu. Bomu la atomiki lina jibu kwa ajili yao, kule, hata hivyo. Hakika linalo. Lakini tuko kwenye wakati wa jioni, saa zilizochelewa kuliko tunavyowazia. Hakika.

142 Hawa Mamajusi, huku na huku mtaani, hawakuwa na jibu. "Imekuwaje? Imekuwaje?" Hatimaye, tunaona ya kwamba walianza kuifuata Hii. Wakati ilipofika kule, wasingeweza kupata—wasingeweza kupata jibu lolote mjini, kwenye milki zao za kidini. La, wala hawapati sasa. Ati wao nini? Yerusalemu, hawakujua kitu juu ya—juu ya ishara yoyote ya kimbinguni.

"Unazungumza juu ya ishara ya aina gani ya kimbinguni?"

143 "Loo, tuliona Nyota wakati tulipokuwa huko nyuma Mashariki. Tunaifuata."

144 "Iko wapi? Siioni. Vema, hatujui lolote kuihusu Hiyo." Ilikuwa ikiyatimiza Maandiko kikamilifu.

145 Lakini hawakuwa na jibu katika jamii zao za kidini. Hawana siku hizi. "Huku kunena kwa lugha ni nini? Kundi hili la watu linaloibuka ni nini, likiwaponya wagonjwa, na kufanya miujiza hii yote na kadhalika, na kupaza sauti, kulia, na mambo haya yote ya namna hii?" Inasikika kama walivyofanya katika Biblia huko nyuma. "Aha, upuuzi. Hakuna kitu Kwake."

146 Hawajui chochote kuhusu mambo ya kimbinguni. Kwa nini? Hii hapa inakuja. Wao hawataifuata ile Nyota ya Nuru, Nyota ya Nuru, dira ya Mungu ya kuelekeza kwenye ile Nuru kamilifu. Loo! "Kuongoza kwenda magharibi, tungali tunaendelea, utuongoze kwenye hiyo Nuru kamilifu, Ee Nyota ya Bethlehemu." Tuliiona Nyota Yake hapa Magharibi. Ni Nyota ya namna gani? Nyota Yake ya kanisa, Roho Mtakatifu, akitenda kazi katika wanadamu. Tumeiona Nyota Yake, nasi tumekuja kumsujudia. Amina. Hivyo ndivyo ilivyo, wanaume wenye

hekima, wanawake wenye hekima, wanyenyekevu moyoni. Tumeiona Nyota Yake, nasi tumekuja kumwabudu.

147 Loo, hawakujua chochote juu ya hayo mambo ya kimbinguni. Hawakujua chochote juu ya Nuru na kadhalika. Wao, wao hawajui chochote kuihusu. Iliwachochea. Hakika. Ndivyo ilivyo siku hizi. Hawakujua chochote kuihusu, hata hivyo. Hiyo jamii ya kidini haikujua. Wala hawajui lolote kuihusu leo hii.

Angalieni. Ninalipenda hili. Loo! Hili ndilo lililo zuri.

148 Ma—maadamu walikuwa katika milki hizo za kimadhehebu, hiyo Nyota kamwe haikuwatokea. Ilizima, kwenye malango ya Yerusalemu, na ikakaa nje. Ndugu! Ikakaa nje, maadamu walipitia kwenye milki hizo za kimadhehebu. "Yuko wapi? Hakika ninyi wachungaji mnapaswa kujua jambo fulani kulihusu. Haya yote yanahusu nini, ninyi marabi na ninyi makuhani? Na nyinyi, nyinyi Wamethodisti, Wabaptisti, Wapresbiteri, Wakatoliki, nanyi makanisa ya kale kama hayo, hakika mnalo jibu Kwake. Yuko wapi?" Loo, jamani! Mnaona? Hawajui chochote juu Yake. Nao waliokuwa mle ndani, walikaa katika giza mpaka walipotoka kwake. Na mara walipotoka humo mjini, hiyo hapo ile Nyota imesimama tena. Utukufu!

149 "Tokeni kwake, enyi watu Wangu," asema Bwana. "Tokeni Babeli, machafuko. Tokeni kwenye kanuni zenu za imani na mambo yenu ya kibinafsi. Nitawapokea," asema Bwana. "Msiguse vitu vyao vichafu," karamu zao za kukiuka maadili kanisani, na karata, na kila namna ya upuuzi, na madansi.

150 Hapa si muda mrefu uliopita, mama yangu aliniita, kasema, "Bill, shuka uje hapa kidogo." Nafikiri ameketi hapa kanisani, mahali fulani, usiku wa leo. Nikashuka huko. Nikasema, "Kuna nini?" Wakaniita kule chini. Na hili hapa lilikuwa kanisa kubwa la Kimethodisti huku juu Indiana, lilikuwa na karamu ya roki mle ndani. Ndipo wakamhoji huyo mchungaji. Akasema, "Kwa muda mrefu kupita kiasi kanisa la Methodisti limeisahau sanaa nzuri ya roki." Amepagawa na pepo! Hajui chochote kumhusu Mungu. Hajui zaidi juu ya Mungu kuliko Mhotentoti angejua juu ya hekaya za Kimisri. Wananinii tu. . . si zaidi ya vile sungura angejua kuhusu viatu vya theluji. Wakati, ninyi mmefikia mahali ambapo jambo pekee mjualo, ni thiolojia tu, kanuni fulani za imani za kujibunia.

151 Wakati Nguvu za Roho Mtakatifu zinapoingia, mnamkubali nabii wa Mungu. Ikubalini Karama ya Mungu ya Roho Mtakatifu, muone mnaweza kuwa na kiasi gani cha roki kanisani. Rudini kwenye Injili ambayo John Wesley alihubiri, muone mnaweza kuwa na kiasi gani mle. Mliondoka kwenye njia zilizoandaliwa; rudini kwa John Smith, ama Wabaptisti, rudini kwa Martin Luther. Lakini ni kitu gani? Hawajui chochote

kuhusu mambo ya kimbinguni siku hizi. Na hiyo ni kweli. Kanisa la Kimethodisti halijui chochote kuhusu uponyaji wa Kiungu.

152 Wakati John alipokuwa amesimama pale, akihubiri uponyaji wa Kiungu, baadhi ya kanisa la juu la Uingereza walikuja na kumdhihaki, wakamwachilia mbweha, na kundi la mbwa wakubwa wa kuwinda. Akamwelekezea kidole usoni mwake, na kusema, "Jua halitatua juu ya kichwa chako, mara tatu, mpaka utakaponiita nikuombee." Akafa jioni hiyo, akimwita John aje amwombee.

153 Kwa nini kanisa la Methodisti lisirudishe Hilo ndani yake tena? Kwa nini? Kwa sababu limekufa. Kweli! Mnaogopa kuangalia ndani ya Kifurushi hicho, maana kitazifunua dhambi zenu. Ninawaita ninyi, Wamethodisti, kuangalia nyuma katika hicho Kifurushi tena. Ninawaita ninyi, Wabaptisti, kuangalia nyuma kwenye Kifurushi hicho tena. Nanyi, Wapresbiteri na wote! Ninyi Wapentekoste, Wakatoliki na wote, angalieni nyuma kwenye Zawadi ya Mungu ya Krismasi sasa. Angalieni nyuma kwenye ile Zawadi. Tupilieni mbali hilo kasha, mkaichukue Zawadi. Uh-huh. Ondokeni kwenye mapambo ya Baba Krismasi. Rudini kwenye Zawadi ya Mungu. Mrudieni Roho Mtakatifu. Loo, ninajua litafunua mambo mengi sana, bali hilo ndilo mnalohitaji, kusafishwa, kusuguliwa kabisa. Ninajua hilo ni gumu sana, jamani, bali hatuna budi kuwa Nalo. Ni Neno la Mungu. Naam, bwana. Ni zuri kwenu. Kweli! Loo, naam!

154 Wao, walijua ya kwamba kulikuwako na kasoro fulani wakati walipofika kwenye mji huo, nayo Nuru ikazima. Mara walipojiunga na dhehebu hili, ile Nuru ilizima. "Kuna nini?" Wakaanza kupaza sauti, "Yuko wapi? Yuko wapi? Hakika nitampata hapa. Hili ni dhehebu la kale, limekuwa hapa muda mrefu. Ndilo makao makuu ya madhehebu, Jiji la Vatikani. Vema, hakika, ninapaswa ku—ninapaswa kumpata hapa. Yuko wapi? Yuko wapi, yule Kristo aliyesema 'Yeye alikuwa ni yule yule jana, leo, na hata milele'? Yuko wapi, Yule aliyesema, 'Itakuwa Nuru wakati wa jioni'? Yuko wapi Yeye aliyesema, 'Kazi nizifanyazo Mimi, ninyi nanyi mtazifanya'? Yuko wapi? Yuko wapi?" Nayo Nuru ilibaki tu imezimika. Wakati walipotoka kwenye kitu hicho, wakatoka nje ya mji, hapo Nuru ilitokea tena.

> Itakuwa Nuru wakati wa jioni,
> Njia ya Utukufu hakika mtaipata;
> Katika njia hiyo ya maji, ndiko kwenye Nuru
> leo hii,
> Kuzikwa katika Jina la thamani la Yesu.
> Vijana kwa wazee, tubuni dhambi zenu zote,
> Roho Mtakatifu hakika ataingia ndani;
> Nuru za jioni zimekuja,
> Ni kweli kwamba Mungu na Kristo ni Mmoja.

155 Naam, ndugu. Naam, bwana. Tubuni dhambi zenu zote. Roho Mtakatifu, Zawadi ya Mungu, hakika ataingia. Yuko mlangoni. [Ndugu Branham anagongagonga mimbarani mfululizo—Mh.] Useme, "Niruhusu niingie. Kama utaniruhusu niingie, nitakula pamoja nawe. Nitayafunua mambo haya kwako. Nitakuonyesha mambo ya kimbinguni. Nitaponya ugonjwa wenu. Nita—nitayashughulikia mambo haya yote kwa ajili yenu, kama mtaniruhusu tu niingie."

156 Kifurushi cha Zawadi ya Mungu, kilichofungwa katika mfano, leo hii, wa Roho Mtakatifu. Kilikuwa kimefungwa, wakati huo, na kuitwa Mwana wa Mungu. Kifurushi cha Zawadi ya Mungu kilikuwa tu kimetwaliwa na kufungwa upya, tena, na kurudishwa. Amina. Kilifungwa katika Mwana wa Mungu, wakati huo. Kimefungwa katika wana wa Mungu, leo hii, wanaoitwa Kanisa. Hiyo ni kweli. Kifurushi cha Zawadi ya Mungu, kimefungwa, kwa watu. Nao walikikataa, leo hii, kama tu walivyokataa wakati ule. "Kama wakimwita Bwana wa nyumba, 'Beelizebuli,' mpiga ramli, kwa sababu angeweza kuyatambua mawazo, ni zaidi sana vipi atakavyowafanyia? Wanamwita Bwana wa nyumba . . . " Loo, jamani! Hebu tuone.

157 Naam, wale Mamajusi, walilipokea. Walikuwa ni maskini na wanyenyekevu, nao walikuwa wameona Nuru ya kigeni.

158 Jambo lingine ninalotaka kulifikia papa hapa. Basi wakati walipoiona Nuru hii, walifurahi kwelikweli! Biblia ilisema, "Walishangilia kwa furaha kubwa mno." Loo, nafikiri walipiga mayowe kidogo, hivi hamfikiri hivyo? Ninawazia hivyo. Kwa hiyo, walipoona wamekuwa kwenye maskini dhehebu hilo la kale muda mrefu huko nyuma, wakijaribu kupata kitu fulani, hapakuwapo na kitu mle, walipotoka nje ya lango, wakaiona ile Nuru ya Roho Mtakatifu tena ikiangaza huko, Nyota ile ya Utukufuni ikimulika chini juu yao, walifurahi sana, walikuwa na furaha kubwa mno.

159 Loo, mtu hufanya nini wanapofurahi kupita kiasi? Mnafanya nini kwenye mchezo wa mpira wanapofurahi kupita kiasi? Loo, mnapiga mayowe, "Huree-huree! Hoyee! Aliingiza goli. Ha-ha! Hu-hu!" Mnaona?

160 Ndipo mnapopata "furaha kubwa mno," na kupiga mayowe, "Utukufu! Haleluya! Bwana asifiwe!" Hiyo ni kweli, furaha kubwa mno! "Ile pale ile Nyota. Tuongoze! Loo, tuondoe kwenye madhehebu haya, na utuongoze kwenye ile Nuru kamilifu. Kutuongoza Magharibi, tungali tunaendelea, utuongoze kwenye Nuru Yako kamilifu." Endelea tu. Ile Nyota ilikuwa iongoze kwenye ile Nuru. Hatimaye, ilikaa juu ya yule Mtoto.

161 Wakati wao . . . [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.] Na dakika chache tu. Vema. Vema.

162 Yeye alijifunua kwa wavuvi maskini. Alifunuliwa. Kifurushi hicho, kile kilichokuwa ndani Yake, kilifunuliwa kwa wavuvi

maskini, kwa wasio na elimu, wasio na kisomo. Alijifunua Mwenyewe kwa watu wasioweza kuandika majina yao wenyewe. Wasingeweza kuwa shemasi, ama—ama chochote kingine kanisani. Wasingeweza kuwa hivyo. Walikuwa wasio na elimu kabisa! Loo, jamani! Walikuwa katika hali mbaya sana! Kwa hiyo Yeye akajifunua Mwenyewe kwao, kwa wasiotakikana, wale ambao walikuwa wametupwa nje. Yeye alijifunua Mwenyewe kwao, kwa wasiopendwa. Yeye alipendeka kwa wale wasiopendwa. Kwa wagonjwa, walihitaji uponyaji. Walikuwa radhi kuangalia katika kile Kifurushi, kuona kuna nini. Yeye alijifunua Mwenyewe kwao. Na kwa wenye njaa, Yeye aliwalisha kwa mikate na samaki. Loo, tungeweza kukaa, nina mambo mengi sana yaliyoandikwa hapa juu ya hilo, bali hatuna budi kuruka hayo. Mnaona? Akajifunua Mwenyewe kwa hao watu wote, wasiopendeka. Wakati hakuna mtu aliyewataka, waliwaita "walokole," Yeye alijifunua Mwenyewe kwao. "Nina furaha sana kwamba ninaweza kusema mimi ni mmoja wao." Naam, bwana! Wasiopendeka, wasiotakikana, wagonjwa na wahitaji, wenye njaa; Yeye alijifunua Mwenyewe. Naam.

163 Nilikuwa nikiwazia juu ya mtu mwingine mwenye njaa. Siku moja, kulikuwako na mtu mwenye njaa moyoni jina lake Paulo, Sauli wakati huo. Alikuwa akienda zake Dameski, yuna njaa. Hakujua la kufanya. Alitaka kumfanyia Mungu jambo fulani. Nuru ilimmulika pande zote, "Sauli, Sauli, mbona wanitesa?" Akajifunua Mwenyewe kwa Paulo mwenye moyo wenye njaa.

164 Kwa mwanamke mwenye sifa mbaya, kwa Baraba aliyehukumiwa, Yeye alijifunua Mwenyewe. Hiyo ni kweli, kwa mtu mwenye moyo wenye njaa, kwa mwanamke mwenye sifa mbaya, kwa hawa wote waliotupwa nje. Ninawazia juu ya yule mwanamke mwenye sifa mbaya. Dakika moja tu kwake, naomba mnivumilie kwa dakika moja tu.

165 Simoni, yule Mfarisayo katika Biblia, loo, yeye alitaka—alitaka kuijua Zawadi hii, pia. Lakini alitaka kuijua kwa mapenzi yake mwenyewe ya kichoyo, malengo yake mwenyewe ya kichoyo. Huyo Farisayo, kwa hiyo alifanya nini? Alikuwa na karamu kubwa. Alifikiri angefanya dhihaka kidogo. Biblia, hadithi ya Injili, inatueleza. Hebu iangalieni kwa dakika moja tu sasa, kabla hatujafunga. Hapo yeye alisema, "Atamwalika Yesu aje." Kwa sababu, sidhani Mfarisayo huyo kweli alimpenda Yesu, maana hakuwa na kitu shirika. Alikuwa ni maskini Mfarisayo mgumu, na a—alimchukia Yesu. Kwa hiyo aliwazia angemwalika kule, na kumfanyia dhihaka kidogo, aone kama kweli Yeye alikuwa ni nabii, ama siye.

166 Kwa hiyo wakatuma ripoti na kumwomba Yeye aje. Tarishi akaja, na kukimbia. Labda amejaa mavumbi, na kila kitu, akaenda pale. Na akasimama karibu na . . . Yesu labda amekuwa akiwaponya watu, na kuendelea. Alikuwa amechoka. Labda ilikuwa ni Petro aliyesema, "Huwezi kumwona leo."

167 Akasema, "Lakini, bwana, bwana wangu ni Rabi Simoni. Yeye ni mchungaji wa kanisa kubwa hapa chini katika Uyahudi. Mbona, wewe . . . Yeye, amemwalika Bwana wenu aje, akamwone. Loo, loo, loo, li—litakuwa ni jina kubwa jinsi gani Kwake. Unaona? Unapaswa kumwona."

168 "Vema," akasema, "nitakupeleka huko, tuone atakayosema." Na kwa hiyo akajipenyeza kupitia kwenye umati. Nalo jua lilikuwa karibu kutua. Yesu, mchovu na amedhoofika. Naye huyu hapa maskini tarishi anakuja. Naye, badala ya . . .

169 Mbele za Kristo! Loo, mara nyingi nimeshangaa tarishi huyo alikuwa na shida gani. Alikuwa na shida gani? Akisimama karibu hivyo na Yesu, na angali alikuwa na ujumbe kutoka kwa yule Mfarisayo, "Bwana wangu anakutaka Wewe uje, ukamwone. Wajua nini? Ana karamu huko chini. Anakutaka uje, uwe mgeni wa heshima."

170 Loo, laiti ningaliupeleka ujumbe huo, ningalikuwa karibu Naye jinsi hiyo, nanyi je? Kamwe nisingaliwazia yale Farisayo huyo aliyosema. Ningalianguka chini miguuni Pake, niseme, "Ee Bwana Yesu, unirehemu, mwenye dhambi." Ninaamini ningalisema hivyo, nanyi je? Jinsi alivyosimama karibu hivyo na Yesu, na hata hivyo akaikataa nafasi ya kumwomba msamaha wa dhambi zake. Huku akiwa karibu Naye hivyo! La, alikuwa na mengi sana niani mwake. Alikuwa ni mtumishi. Ilimbidi kuomba kwa niaba ya huyo Mfarisayo.

171 Naye Yesu, maskini Yesu, huku ni mchovu na amedhoofika, na akijua kwamba alidharauliwa na kuchukiwa naye, Yeye alikitikisa kichwa Chake, "Nitakuwako." Anaposema atakuwako, atakuwako. Msiwe na wasiwasi. Atakuwako. Hakuna kitu kitakachomkomesha.

172 Kwa hiyo wakati walipofika kule chini, siku hiyo, nao wakachinja ndama wao wote walionona, na wakaleta divai yao yote mpya na kila kitu. Nao watu maskini hawakuruhusiwa kukaribia mahali walipokuwa. Loo, walipoichoma nyama hiyo huko nje, viungo, ni harufu ya jinsi gani! Hao watu maskini walisimama huko nje, huku wakimeza mate tu. Wasingeweza kuingia. La, bwana. Hata hivyo, hiyo ilikuwa tu ni kwa watu mashuhuri pekee. Na kwa hiyo basi wakasimama nje. Nao walikuwa na zabibu hizi zote na kadhalika, zote katika wa—wakati wenyewe wa kuchanua, ama utimilifu wa zabibu. Na harufu hiyo nzuri ya zabibu, mwajua, wakati zikiwa ni tamu, na kila kitu. Yeye alikuwa na divai zake mpya na kadhalika.

173 Na mimi mara nyingi nimeshangaa jinsi Yesu alivyoingia kule pasipo kuonekana. Mwajua, vema, wakati mtu yeyote huko Mashariki kamwe akikualika uje nyumbani mwao, unajua wao ni watu wakarimu sana. Sasa, watu katika siku hizo, wakati walipotembea, walikuwa na makubadhi. Nao walipozivaa, mnasikia kuhusu kutawadha miguu.

174 Hivyo ndivyo tunavyofanya hapa, katika kumbukumbu. Hilo lilikuwa ni agizo.

175 Wakati mtu alipokualika kuja nyumbani mwao, ingekuwa ni kitu kama hiki. Wangekusalimu mlangoni. Kisha walikuwa na kile walichoita, "kazi duni kabisa," ya watu wote. Baadhi yao waliendesha magari ya farasi. Baadhi yao walipika. Na baadhi yao, wapishi, mwajua. Na baadhi yao, wanyweshaji. Na, ila mtu mwenye mshahara mdogo kuliko watu wote nyumbani, alikuwa ni mtawadha miguu. Alikuwa tu ni mtawadhaji.

176 Basi, wazieni, Bwana wangu alikuwa ni mtawadha miguu. Halafu sisi tunawazia jambo fulani, tunafikiri sisi ni mtu maarufu. Hebu mwangalieni Yeye akiwatawadha wanafunzi miguu, wavuvi, wavuvi wachafu, wachunga kondoo na kadhalika, aliwatawadha miguu.

177 Na, hapa, huyo mtawadha miguu. Ulipofika mlangoni, wange—wangekutawadha miguu, kwa sababu mavumbi na kadhalika yaliingia miguuni mwako, na—na mahali ulipotembelea, wajua, kupitia kwenye barabara za mavumbi ambamo farasi na wanyama wamepitia, mwajua. Nayo ilitoa harufu mbaya, mwilini mwako mwote. Halafu jua hilo, wajua, lilikuwa kote shingoni mwako. Nalo hilo jua la Palestina, miali yake ya moja kwa moja, kweli ina joto. Na kwa hiyo walipofika mlangoni, waliinyosha miguu yao. Wangewatawadha miguu yao. Kisha wanaweka—wanaweka makubadhi yao juu; wanayasafisha, na kuyaweka juu. Ndipo wanawavalisha maskini jozi ya ndara, kama maskini ninii . . . wanazovaa wanawake siku hizi kama ndara za chumba cha kulala, mwajua, kitu kama hicho, wakazivaa. Kisha kutawadhwa miguu.

Halafu wangekuwa na taulo begani mwake. Ndipo basi kile angefanya, angepangusa mavumbi usoni mwake.

178 Kisha achukue manukato ya mafuta. Loo, yalikuwa ni viungo vya bei kubwa ambavyo matajiri walitumia. Malkia wa Kusini alileta baadhi yake na kumpa Sulemani, yaliyotengenezwa kwa tofaa huko Mashariki. Kama vile ua, lile tofaa dogo la ua, nalo hutolewa humo. Ghali mno.

179 Nao wanayachukua manukato hayo, na kujipaka kote usoni mwao. Mafuta kama hayo, maana shingo zao zilibabuka, na kadhalika. Wanachukua taulo na kuyapangusa yote, namna hiyo. Ndipo basi wali—waliburudika.

180 Sasa, hilo ndilo jambo la kwanza, mtawadha miguu aliwachukua na kuwashughulikia namna hiyo. Hakika, wasingejisikia kuingia nyumbani mwa mtu, ambapo hayo mazulia makubwa mno ya Uajemi, na kadhalika, namna hiyo, wakinuka kana kwamba walikuwa katika zizi, na—na—na jua na malengelenge kote usoni mwao. Waliburudika.

181 Ndipo walipoingia, walikutana mmoja na mwingine. Basi walipokutana, daima kumkaribisha mgeni, ambapo kama

ulikaribishwa, walipeana mikono namna *hii*, Ndugu Ed. Wangepeana mkono, namna *hii*. Halafu basi wakaweka ninii yao. . .Hebu simama, kwa dakika moja tu, nitakuonyesha jambo fulani. Wanawakumbatia kwa mikono. [Ndugu Branham anaonyesha kwa mfano, na kupigapiga Ndugu Ed mara nne—Mhariri.] Namna *hiyo*, kisha wanabadilisha mikono. [Ndugu Branham mara nyingine tena anampigapiga Ndugu Ed mara nne.] Basi hivyo ndivyo walivyofanya.

182 Hilo lilikuwa karibisho. Ndipo ulikuwa ni ndugu. Ukajisikia vizuri. Miguu yako ilitawadhwa. U—ulipakwa mafuta kila mahali.

183 Halafu basi jambo lingine alilofanya, walibusiana shingoni. Na hilo liliwafanya kujisikia wamekaribishwa. Kitu hicho cha mwisho kilikuwa ni hilo busu la makaribisho.

184 Mnakumbuka Yuda akimpa Yesu hilo busu la makaribisho? Kasema, "Kwa nini ukafanya hivyo, rafiki?" Mnaona? Yeye aliujua moyo wake.

185 Kwa hiyo walikaribishana. Hukujisikia kuingia ukiwa na mavumbi mwilini mwote, na maskini harufu hiyo mbaya usoni mwako mwote na miguuni, na kadhalika. Vazi hilo la kale lilining'inia chini, likaokota mavumbi hayo wakati ukitembea, wakati ulipokuwa ukitembea. Hawakujisikia kufanya hivyo, kuingia ndani. Lakini wakati umeburudika kabisa, halafu basi wakati akija, na mgeni wako. . .Ulikuwa ni mgeni wa heshima, halafu basi wakati alipokuja na kukukaribisha, na kukupa busu shingoni, mbona, ulikuwa ndugu basi. "Karibu. Nenda kwenye friji, jitwalie sambusa, chochote." Ulikuwa—ulikuwa umekaribishwa basi. Ulikaribishwa ndani.

186 Lakini Yesu aliingiaje humu pasipo kufanyiwa hayo yote? Mnaona? Alikuwa ameketi pale pembeni, na miguu michafu, hajakaribishwa. Labda, Mfarisayo alikuwa akizungumzia jambo lingine, mwajua. Kamwe hakumwona Yesu akiingia.

187 Hiyo ndiyo shida makanisani siku hizi, mengi sana ya makanisa yetu ya Kifarisayo. Nguvu za Mungu zinaingia, wala hawazioni Hizo. Mnaona? Yeye angekuwa tayari kufanya jambo fulani, bali kamwe hakaribishwi.

188 Naye huyo pale, huko, labda akifanya mizaha, na akiwa na wakati mzuri pamoja na Mchungaji Rabi *Nanii wa nanii* na Rabi *Nanii wa nanii,* kule. Hawakumwona Yesu.

189 Naye hapana shaka aliingia kisiri na kuketi chini mahali fulani, pale pembeni. Ninaweza kumwona pale na miguu Yake michafu, shingo iliyojaa malengelenge, hakuna busu la makaribisho. Loo, hilo haliwafanyi kujisikia kigeni, Yesu akiwa na miguu michafu? Wanamwita, kule, "Jezu! Jezu!" Kasema, "Jezu mwenye miguu michafu, ameketi pembeni." Ee Mungu, ingewezekanaje? Hakuna mtu anayemjali.

190 Lakini maskini kahaba mmoja, (loo, jamani) mwanamke mwenye sifa mbaya, ilitokea alipitia pale, labda yeye—labda yeye alikuwa . . . Hakuna mtu mjini. Kila mtu alikuwa ameenda kwenye karamu hii, watu wote mashuhuri, kwa hiyo biashara yake ilikuwa imeshuka. Kwa hiyo, akaona. "Ni nini haya yote hapa juu, kwenye hii, hapa juu nyumbani mwa Mfarisayo, yanahusu nini?" Kwa hiyo akaenda pale juu, na labda kuangalia kwenye ufa wa ua, akiangalia kote. "Loo, jamani!" Ilitokea aliangalia huko pembeni. Akamwona ameketi pale, amekiinamisha kichwa Chake, miguu michafu, shingo yenye malengelenge, hajakaribishwa, hakuna anayemjali.

191 Lakini ilifunuliwa kwake. Loo, ninaweza kumwona akiyapangusa macho yake, na kusema, "Yule ni Yeye? Yule ni Mtu yule yule aliyemwachilia mwanamke kama mimi tu, wakati mmoja, wakati alipokokotwa nje na lile kanisa, nao walikuwa wakitaka kumpiga mawe hata afe. Naye akasema, 'Mwanamke, washtaki wako wako wapi?' Hapana shaka yule Ndiye." Mnaona? Imani chanzo chake ni kusikia, ndipo ikafunuliwa kwake kwamba huyo alikuwa Ndiye.

192 Akasema, "Lakini, angalia, hajakaribishwa. Yuna miguu michafu. Nifanye nini kulihusu? Mimi ni mwanamke, na kama ikitokea niingie mle na kusema kitu, mbona, wa—wangenitupa huko nje juu ya zile fito. Sasa, mimi ni—mimi ni mwanamke mwenye sifa mbaya, na Yeye—Yeye angejua nilikuwa na sifa mbaya. Angejua nilikuwa mwanamke mbaya, kwa hiyo nifanye nini juu yake?"

193 Ninaweza kumwona akigeuka, anatembea huku na huku, anasema, "Loo, sina budi kufanya jambo. Yeye hajakaribishwa. Lakini kitu Fulani kinanifunulia ya kwamba hiyo ndiyo njia pekee nitakayoweza kupata Uzima." Haya basi. Loo, ndugu. "Ninataka kuona ni nini kilicho ndani ya Kifurushi hicho. Najua kuna kitu Fulani mle ndani kitakachonisamehe dhambi zangu. Ingawa mimi ni kahaba, ingawa mimi ni mwovu, ninataka kuangalia kwenye kile Kifurushi cha Krismasi. Ninajua kuna kitu Fulani mle kwa ajili yangu."

194 Kuna kitu Fulani kwa ajili ya kila mtu. Hiyo ni kweli, rafiki mwenye dhambi. Kuna kitu Fulani kwa ajili ya mcheza kamari. Kuna kitu Fulani kwa ajili ya mwongo. Kuna kitu Fulani kwa ajili ya kila mtu. Kuna kitu Fulani katika Kifurushi hiki cha Krismasi, kwa ajili yako. Usikitupe kando. Jinsi ambavyo Mfarisayo, yule punguani mjinga, alivyochukua mapambo na kuitupilia mbali ile Zawadi! Ni jambo la kusikitisha jinsi gani!

Huyu hapa anakuja. Ameketi pale.

195 Naye maskini mwanamke huyu, labda anaenda kwenye nyumba anamoishi, anapanda vipandio vya kale vinavyoalika huko juu. Anashika soksi yake ndefu, ama kitu kingine na kuchukua pesa. Akasema, "Loo, nifanyeje? Sasa ngoja kidogo,

afadhali nizirudishe hizi, kwa sababu Yeye atajua kwamba mimi—mimi ni mwanamke mwenye sifa mbaya. Lakini ndilo tumaini langu la pekee, ndilo jambo pekee ninaloweza kufanya. Sijaalikwa kwenye karamu hiyo, lakini hata hivyo sina budi kwenda Kwake."

196 Loo, laiti watu wangeweza kuona hilo usiku wa leo. Nenda Kwake, la sivyo uangamie. Inaleta tofauti gani, kama unaitwa "mtakatifu anayejibingirisha," ama kutupwa nje, ama kuna tofauti gani? Nenda Kwake. Nenda Kwake, hilo ndilo tumaini lako la pekee.

197 Akashuka, akachukua hii. Ninaweza kuona mmoja, hao jamaa wa Kiyahudi kule, akisema biashara imekuwa mbaya, ameketi pale, akihesabu pesa zake. Kila mtu ameenda kwenye ile karamu, na kila kitu. Mwanamke huyu akaingia. "Vema, unafanya nini humu ndani?" Akazimwaga hizi dinari za Kirumi kwenye kaunta, yapata vipande thelathini vyake. "A-ha! Unataka nini, mama?" Mnaona, hilo lilileta tofauti. Yeye aliona alikuwa ni nani; lakini wakati alipoona alikuwa na pesa, hiyo ni tofauti. Unaona? Huo ndio ulimwengu, siku hizi. Ukiwa na pesa, wewe ni mtu mkubwa. Usipokuwa nazo, wewe—wewe si kitu. "Loo, hiyo ni tofauti. Unataka nini?"

198 "Na—nataka yaliyo mazuri kuliko yote, manukato mazuri kuliko yote uliyo nayo. Hizi tu ndizo nilizo nazo. Hebu nizihesabu, vipande thelathini. Kulikuwa na arobaini."

"Loo, naam, hizo zitanunua chupa hii papa hapa, yaliyo mazuri kuliko yote."

"Ninayataka."

"Unamaanisha unataka kununua mafuta?"

"Ninayataka. Ninataka chupa hiyo yote." Hizo tu ndizo alizokuwa nazo.

199 Hivyo ndivyo inavyokupasa kufanya, ndugu. Inagharimu kila dhambi uliyo nayo. Inagharimu kila kitu. Lakini uwe tayari kuitoa.

200 Kwa hiyo anajipenyeza uani. Ninaweza kumwona akiangalia mle ndani. Anamwona ameketi pale, angali hajaguswa. Naye yule mchungaji Mfarisayo angali anafanya mizaha yake michafu na kadhalika, huko pamoja na hao wengine, wakipiga makelele, wakizungumza kuhusu mambo makuu mahali fulani, pasipo kujua, bila kuonekana na Bwana we—wetu wa thamani. Akasema, "Ninawezaje kuingia?" Kwa hiyo sasa ninamwona akiingia kisiri sana, anafika mahali Yeye alipo namna hiyo. Ndipo akamwangalia. Ninaweza kumwona huku machozi yakitiririka usoni mwake, na macho yake makubwa ya hudhurungi yakimwangalia namna hiyo. Ndipo upesi akaifungua ile chupa, akayafungua hayo manukato,

akayamwaga miguuni mwake. Asingemwacha Yesu aketi na miguu michafu.

Unasema, "Nisingemwacha pia."

201 Kwa nini usifanye jambo kulihusu basi? Yeye ana jina baya kuliko yote lililopo nchini leo hii, "mtakatifu anayejibingirisha, shupavu wa dini." Kwa nini usifanye jambo fulani kulihusu? Usimame na kusema, "Nitashika njia na wachache wa Bwana waliodharauliwa. Niko tayari kupokea Kifurushi hicho."

202 Akayamwaga yale mafuta miguuni Mwake. Chumba chote kikametameta kwayo. Yalikuwa ni ya bei kubwa.

203 Hakuna kitu kilicho kizuri kupita kiasi kwa Yesu. Mpe chako kilicho bora kuliko vyote. Mpe kila kitu ulicho nacho. Maisha yako, nafsi yako, utu wako, wakati wako, yote uliyo nayo, mpe Yeye.

204 Ndipo ikatokea aliangalia. Alikuwa amesimama pale. Loo, jamani! Akayamwaga mafuta haya kichwani Mwa—Mwake. Kisha akaishika miguu Yake, na kuanza. Loo! A—akaiinua miguu Yake, na kuangalia, ilikuwa michafu. Hakuwa na kitu. Ndipo a—akaanza kuwazia juu ya dhambi zake, naye akasema, "Hakika, Yeye, Yeye ata—Yeye atanihukumu." Kwa hiyo wakati alipompaka mafuta shingoni Mwake, na kuisugua, ndipo akainama hapo na kuishika miguu Yake.

205 Ndipo akaanguka chini. Akaanza kulia, "Loo, mimi ni mwenye dhambi sana, kusimama mbele ya Mtu huyu. Mimi ni mwenye dhambi sana." Ndipo akaangalia juu, nayo macho yake makubwa, mazuri. Akawazia, "Yeye—Yeye yuko karibu kunipiga teke nitoke humu chumbani." Lakini, Yeye hakusogea. Aliketi tu na kumwangalia. Loo, napenda jambo hilo. Aliketi tu na kumwangalia. "Loo, Yeye anaujua moyo wangu. Ninaweza kumhisi sasa hivi akisoma kwenye kilindi cha nia yangu. Yeye anajua mimi si mwema. Ninajua hilo, Bwana, bali siwezi kuvumilia kukuona ukiwa na miguu michafu. Kamwe siwezi kuvumilia. Wewe ndiwe tumaini langu la pekee. Siwezi kuvumilia hilo." Ni maji mazuri jinsi gani kwa ajili ya miguu Yake, loo, machozi ya toba! Loo! Loo! Maskini Farisayo wa kale asingeweza kutoa kitu cha namna hiyo. Maji, machozi yakitiririka mashavuni mwake.

206 Naye akaanza kuipangusa, na "*busu*, *busu*," miguu Yake. Loo, ilikuwa ni Bwana wake! Akiibusu miguu Yake. Yeye hakuwa na—hakuwa na taulo ya kuipangusia. Kwa hiyo nadhani mawimbi ya nywele zake, alikuwa ameyakusanya juu ya kichwa chake, hapana shaka yalianguka chini, kote. Akazishika nywele zake, akaanza ku—kuipangusa miguu Yake kwazo, *busu*, huku anaibusu miguu Yake. "Bwana, Wewe wajua, *busu*, Bwana, Wewe wajua mimi—mimi ni mwenye dhambi, Na—nachukia kuwa hapa mbele Zako namna hii, bali siwezi kuvumilia kukuona ukiwa na miguu michafu." Loo, jamani! Yesu akiwa na miguu

michafu, hajakaribishwa, hakuna busu shingoni, yeye alikuwa hata akiibusu miguu Yake. "Bwana! *Busu*, *busu*, *busu*, Ee Bwana! Ee Bwana, mi—mimi—mimi ni mwenye dhambi, busu, busu, Wewe unajua ndivyo nilivyo, Bwana."

207 Na yapata wakati huo, maskini Farisayo akageuka. "Huh!" Kasema, "Sasa angalieni kule. Angalieni kule. Hilo ndilo kundi lililo na Kile kinachoitwa Roho Mtakatifu." Mnaona? Hawajabadilika. "Angalieni kile kilicho. Angalieni Yeye anashirikiana na watu wa namna gani. Mnazungumza juu ya huyo Roho Mtakatifu, na uponyaji wa Kiungu, ni Kitu gani? Takataka ya mjini."

208 Hakika, hao ndio wanaofunuliwa Hayo. Yeye alijua kilichokuwa kwenye Kifurushi hicho. Yeye alijua wakati wa pekee kuliko wakati wowote angaliweza kufika popote... Yeye asingalishuka kwenda kwa Mfarisayo, yeye angemfukuza kanisani; sio kwenye shirika lao la jamii. Lakini kulikuwa na Shirika kwa ajili ya mwenye dhambi. Nina furaha sana kwa ajili ya jambo hilo. Kuna Mahali ambapo mwenye dhambi anaweza kuja. Kuna Zeri katika Giliadi, itakayowapoza waliojeruhiwa. Yeye alikuwa ameipata. Alitaka kujua Zawadi hiyo, naye alikuwa akiibusu miguu Yake.

209 Maskini Farisayo akasema, "Ah-ah! Njoni hapa, jamani. Huh! Uh! Yule pale Nabii wenu. Mnaona? Kama angalikuwa namna yoyote ya Nabii, Yeye angejua ni mwanamke wa namna gani anayeitawadha miguu Yake. Angalieni pale. Nena kuhusu ulokole? Linaleta aibu nyumbani mwangu."

210 Yesu kamwe hakusema neno, alisimama tu na kumwangalia huyo mwanamke. Kwa hiyo baada ya kitambo kidogo... Yeye alijua yale Mfarisayo mwenye akili timamu aliyokuwa akiwazia, kwa hiyo akasimama.

211 Mwanamke huyo, ninaweza kumwona, "Loo! Loo, huu—huu hapa wakati wangu. Yeye—Yeye—Yeye, Yeye ata—Yeye atanihukumu. Yeye ata—Yeye ata—Yeye atanifukuza kwenye nyumba hii." Ninamwona amesimama, akiangalia namna *hiyo*. Anajisikia vizuri sana sasa; miguu Yake imetawadhwa kwa machozi. Ee Mungu, yachukue yangu. Miguu Yake imetawadhwa kwa machozi ya toba, moyo wa kweli. Ingawa ni mtovu wa uadilifu, kama alivyokuwa, huu ndio wakati pekee aliopata kuwa kwenye chemchemi ambamo angeweza kuoshwa awe safi. Hapo, ameketi pale. Usoni, ninaweza kumwona na machozi yaliyotiririka usoni mwake namna hiyo, amechafuka kila mahali. Nywele zake zilizotiwa mawimbi zote zimeshushwa chini, na zimejaa machozi na uchafu kutoka kwenye miguu Yake. Alikuwa amesimama pale, akishangaa, "Itakuwaje? Atanitupa nje. Atawafanya wanitie korokoroni kwa sababu ya kuja hapa."

212 Akasimama, namna *hiyo*. Akasema, "Simoni, nina Neno ninalotaka kukwambia. Ulinialika nyumbani mwako. Na wakati

nilipoingia, hukunipa maji yoyote kwa ajili ya miguu Yangu. Ningalikuwa nimeitawadha Yangu Mwenyewe, bali kamwe hukunipa maji." Ee Mungu! "Hukunipa mafuta yoyote, kupaka shingo Yangu, wakati ilikuwa ikichoma. Hukufanya hivyo, Simoni. Wala hukunibusu na kunikaribisha Mimi. Lakini mwanamke huyu, yeye ameiosha miguu Yangu kwa machozi yake. Pia ameibusu miguu Yangu, wala hajaacha kufanya hivyo tangu alipokuja hapa ndani. Ninayo mambo machache dhidi yako, Simoni. Lakini yeye. . . " (Hivi alikuwa Nabii, au la?) "Ninamwambia, dhambi zake zilizo nyingi zimesamehewa." Ee Mungu!

213 Ilikuwa ni kitu gani? Yeye alipata kile kilichokuwa kwenye Kifurushi hicho cha Zawadi. Aliona kulikuwako na upendo. Aliona kulikuwako na msamaha. Alikuwa ameona Hilo. Loo, jinsi alivyoona ile Zawadi ya thamani ya Mungu ikitenda kazi juu yake! Jinsi hapana shaka ilimfanya kujisikia hapo alipoona Zawadi hiyo ya Mungu ikielekezwa kwake! Dhambi zake zilisamehewa.

214 Jinsi Baraba hapana shaka alijisikia siku hiyo! Mnamjua Baraba, ile simulizi. Baraba ni yule mhalifu aliyeshikwa, naye akawekwa manchani, alikuwa afe kesho yake asubuhi. Alikuwa ni mwizi. Alikuwa haramia. Alikuwa mwuaji. Alikuwa mhalifu. Ndipo usiku kucha alitembea huku na huku kwenye gereza hilo, akizivuta nywele zake, kwa kuwa, kesho yake asubuhi aliende kwenye msalaba, hukumu ya kifo. Angekufa. Jinsi ambavyo jinamizi zilipitia juu yake usiku huo! Jinsi ambavyo asingeweza kupumzika!

215 Ndipo kesho yake asubuhi, hakuna kiamshakinywa wala chochote, alijua damu yake ingetiririka kama miongoni mwa mbwa mwitu. Mara, anasikia minyororo ikichacharisha. [Ndugu Branham anaigiza askari wakitembea taratibu—Mh.] Ni vishindo vya askari. Hawa hapa wanne ama watano wanakuja, na labda ba—batalioni ya askari wa Kirumi, mikuki ikimetameta, wakaenda pale. Yule mlinzi mkuu wa jela akaingiza ufunguo, na kusema, "Toka nje, Baraba."

"Loo, msiniue! Mnirehemu!"

"Baraba, hakuna shida. Uko huru."

"Ati nini?"

"Uko huru."

"Kwani nimekuwaje huru?"

216 Mtu fulani akaelekeza kidole *huko*. Kile hapana shaka lilimaanisha kwa Baraba, wakati alipoiona ile Zawadi ikipachukua mahali pake katika mauti. Nilijisikia vile vile, Zawadi ya Mungu ilichukua mahali pangu katika mauti. Jinsi, yule mwivi aliyekuwa akifa msalabani, ametundikwa kule juu:

Mwivi anayekufa alifurahia kuona
Chemichemi hiyo katika siku yake;
Hapo nijalie mimi, ingawa ni mwovu kama yeye,
Kuziosha dhambi zangu zote. (Naam.)

Tangu kwa imani nilipokiona Kijito kile, (kilichofunuliwa kwangu,)
Kilichotoka kwenye majeraha Yako,
Upendo wa ukombozi umekuwa ndio wimbo wangu,
Na utakuwa hata nitakapokufa. (Hiyo ni kweli. Loo!)

217 Kufunga, huenda nikasema jambo hili. Leo hii, Krismasi inamaanisha pakiti ya sigara za Camels, pakiti ya Viceroy, chupa ya Four Roses ama Seagramu, zilizofungwa kwenye karatasi nzuri ya Baba Krismasi. Lakini wangali wanaikataa Zawadi ya Mungu ya Krismasi. Wangali wanaikataa Zawadi Yake ya Krismasi. Hawaitaki.

218 Ninaitaka mimi. Nina furaha niliipokea. Ee Imanueli, Mungu aliyefanyika mwili akakaa miongoni mwetu, aliyekataliwa na kuhukumiwa, kote katika nyakati, nayo rehema Yake inatolewa leo hii kwa kila moyo utakaompokea Yeye.

Hebu tuinamishe vichwa vyetu kwa dakika moja.

219 Nashangaa, usiku wa leo, katika jengo hili, kwenye wakati huu wa Krismasi, katika kumbukumbu ya karibu miaka elfu mbili iliyopita, wakati Mungu alipotoa Zawadi ya kwanza ya Krismasi. Nashangaa, usiku wa leo, kama ungetaka kuangalia ndani ya Kifurushi hicho na kuona, mwenye dhambi, ya kwamba hakuna Mtu mle ndani Ambaye anakupenda, Mtu fulani Ambaye alikufa kwa ajili yako, Mtu fulani aliyetoa maisha Yao kwa ajili yako? Ungekuwa radhi, usiku wa leo, kumwondolea nguo za kitoto kutoka Kwake, hiyo nguo chafu wanayomwita Yeye, "mlokole na mtakatifu anayejibingirisha," ujifunike nayo, na kushika njia pamoja na wachache wa Bwana waliodharauliwa?

220 Kama umo humu jengoni, usiku wa leo, ungetaka kukumbukwa katika maombi, ungeweza tu kuinua mkono wako, useme, "Kwenye usiku huu wa Krismasi, ninataka kupokea Zawadi ya Mungu ya Krismasi, Zawadi ya kweli ya Mungu ya Krismasi"? Mungu akubariki, mama. Mungu akubariki, msichana. Mungu akubariki dada. Mungu akubariki. Mungu ambariki huyo msichana hapo. Naam. Huenda kuna wengine, wangetaka kukumbukwa katika maombi? "Bwana . . . " Mungu akubariki, ndugu yangu.

221 Mtu mwingine, "Bwana, nitaichukua hiyo njia. Wala, kamwe sitakuona umeketi na miguu michafu. Kamwe sitavumilia . . . Nitajiunga nao. Nitaingia moja kwa moja katika Ufalme wa

Mungu. Nita—nitakuwa mmoja wa hao waliodharauliwa. Kaa nami, Bwana. Njoo, nenda nyumbani pamoja nami, usiku wa leo. Nitaosha uchafu wote kutoka kwenye Jina Lako. Wewe zioshe dhambi zangu, Bwana, jalia niishi Maisha, sio vile ninavyoishi sasa; ninayachafua Yako. Ni—ninakuchafua, kila siku, nikiweka mwingi zaidi juu Yako. Jalia niende, usiku wa leo, Bwana, na pamoja na machozi yangu ya toba, sasa ninakuja kwa unyenyekevu chini ya msalaba, kukupokea Wewe kama Mwokozi wangu." Kuna mwingine kabla hatujaomba? Inua tu mkono wako. Vema.

222 Bwana wa thamani, tunakuletea Wewe, usiku wa leo, inaonekana kana kwamba ilikuwa ni wanawake kiasi, usiku wa leo, Bwana, walioinua mkono wao. Labda wao pia wanaweza kuangalia chini. . .Baadhi yao ni wasichana wadogo, matineja tu, walioinua mikono yao. Hao, wanamaanisha hilo, Bwana. Hawataki—hawataki kuhukumiwa pamoja na ulimwengu. Wanataka kukupokea sasa, wakati huu wa Krismasi, kuangalia katika Kifurushi cha Mungu, na kupokea Uzima wa Milele. Lijalie, Bwana, sasa hivi, ya kwamba utawafungulia msamaha wa dhambi zao, kwamba utawafungulia Chemchemi katika nyumba ya Daudi, ambayo imefunguliwa kwa dhambi na uovu, ambapo wenye dhambi wakitumbukia chini ya hiyo gharika, hupoteza waa lao la dhambi. Tujalie, Bwana. Nenda nyumbani pamoja nao, na ukae pamoja nao, usiku wa leo, Bwana. Fanya maisha, kwao, yanavyopaswa kuwa, Bwana. Tujalie.

223 Waponye wagonjwa na wanaoteseka miongoni mwetu. Wewe ndiwe Msaada wa wasiojiweza. Wewe Ndiwe, Bwana, Ambaye anaweza kutenda ambapo wengine hawawezi. Wewe ni Neema idumuyo. Wewe ni Zawadi ya Mungu. Nasi kwa unyenyekevu tunakuamini Wewe, Bwana. Tunaifuata Nyota ya Siku, tunaifuata Nuru mpaka itakapotuongoza kwenye Nuru hiyo kamilifu, Zawadi ya Mungu, Uzima wa Milele, kwa ubatizo wa Roho. Tujalie, Bwana. Ninawakabidhi Kwako sasa. Katika Jina la Yesu Kristo, zichukue nafsi zao usiku wa leo, na uzioshe katika Damu nyekundu ya Kalvari. Kwa kuwa tunaomba katika Jina la Yesu. Amina.

> Bwana, kaa nami.
> [Ndugu Branham anavumisha *Kaa Nami*—Mh.] . . .-shindwa kunifariji,
> Katika maisha, katika mauti, Ee Bwana, kaa nami.

224 Mnampenda kwa moyo wenu wote? Mara nyingine tena, kwa ajili ya wakati wa kale, "Nampenda, nampenda kwani alinipenda kwanza." Kila mtu sasa.

> Nampenda
> Kwani Yeye . . .

Na tumwinulie mikono yetu.

Na kununua wokovu wangu
Mtini Kalvari.

225 Sasa, ninawatakeni kupeana mikono na mtu fulani mbele yako, na nyuma, na kando yako, sasa.

Nampenda, nampenda
Kwani alinipenda kwanza
Na kununua wokovu wangu
. . . Kalvari.

226 Wote walioipokea Zawadi ya Krismasi ya Mungu, inueni mikono yenu sasa.

Nampenda, nampenda
Kwani alinipenda kwanza
Na kununua wokovu wangu
Mtini Kalvari.

227 Hivi hamumpendi Yeye? Yeye si ni wa ajabu? Vema, wakati tukisimama sasa:

Peleka Jina la Yesu,
Mtoto wa huzuni na majonzi;
Litakupa furaha na faraja,
Lipeleke kokote uendako.

Jina la thamani, Loo ni tamu jinsi gani! (Loo, ni tamu jinsi gani!)
Tumaini la duniani na furaha ya Mbinguni;
Jina la thamani, (Jina la thamani!) Loo ni tamu jinsi gani!
Tumaini la duniani na furaha ya Mbinguni.

Polepole sasa:

Peleka Jina la Yesu,
Kama Ngao dhidi ya kila mtego;
Wakati majaribu . . . (Unafanya nini wakati majaribu yanapokusanyika?) . . . kusanyika,
Litamke tu Jina hilo Takatifu katika maombi.

Jina la thamani, (Jina la thamani!) Loo ni tamu jinsi gani! (Loo ni tamu jinsi gani!)
Tumaini la duniani na furaha ya Mbinguni;
Jina la thamani, (Jina la thamani!) Loo ni tamu jinsi gani!
Tumaini duniani na furaha ya Mbinguni.

Katika Jina la Yesu . . .

Hebu tuinamishe vichwa vyetu na kuimba.

. . . inamia,
Tukisujudu miguuni Pake,
Tutamvika taji Mbinguni Mfalme wa wafalme,
Safari yetu itakapokamilika.

Jina la thamani, Loo ni tamu jinsi gani! (Tamu jinsi gani!)
Tumaini la duniani na furaha ya Mbinguni;
Jina la thamani, Loo ni tamu jinsi gani!
Tumaini duniani na furaha ya Mbinguni.

Zawadi Ya Mungu Iliyofungwa SWA60-1225
(God's Wrapped Gift)

Ujumbe huu uliohubiriwa na Ndugu William Marrion Branham, uliotolewa hapo awali katika Kiingereza kwenye asubuhi ya Jumapili ya Krismasi, tarehe 25 Desemba, 1960, katika Maskani ya Branham huko Jeffersonville, Indiana, Marekani, umetolewa kwenye kanda ya sumaku iliyorekodiwa na kuchapishwa bila kufupishwa katika Kiingereza. Tafsiri hii ya Kiswahili ilichapishwa na kusambazwa na Voice Of God Recordings.

SWAHILI

©2021 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org

Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org